# Nipashe

Jumatatu Julai 29, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579982

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Daktari aeleza hatari ya kumrusha mtoto mchanga

UKURASA 21




UKURASA 13


# Udukuzi mawasiliano waibua wanaharakati

**WATAKA** itungwe sheria kulinda faragha za watu, walioguswa washauriwa kufungua kesi mahakamani...*Endelea ukurasa wa 2*



Meneja wa Mgodi wa Tanzanite Afrika, Wilfred Mushi, akizungumza jambo jana eneo la Mirerani wilayani Simanjiro na Waziri wa madini Dotto Biteko, katika eneo la migodi ya Tanzanite. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Sugu alia polisi kuzuia mikutano



UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### AFARIKI AKICHIMBA UDONGO WA KUJENGEA

MKAZI wa kijiji cha Nyambui Kata ya Tinde wilayani Shinyanga, Hassan Tundu (26), amefariki dunia...

UKURASA WA 3

### ACT-WAZALENDO YATAMBA KUNYAKUA MAJIMBO ILALA

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama chake kimejiandaa kushinda...

UKURASA WA 5

### WATALII WAINGIZA TRILIONI 4. 5/-

SERIKALI imesema idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka hadi kufikia milioni 1.5 kutoka milioni...

## Lugola amng'oa Mkuu wa Trafiki

UKURASA 3

MICHEZO ZFCA YAFANYA MAREKEBISHO YA KATIBA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipokea misaada mbali mbali yenye thamani ya milioni 25 kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali NMB, Vicky Bishubo katika hafla iliyofanyika wilayani Ruangwa mkoani Lindi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Udukuzi mawasiliano waibua wanaharakati

**Na Enock Charles**

ZIKIWA zimepita siku kadhaa tangu kutolewa madai ya kudukuliwa mawasiliano ya viongozi wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Serikali imetakiwa kutunga sheria madhubuti juu ya haki ya faragha katika mawasiliano.

Pia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imetakiwa kuhakikisha watoa huduma wanaondoa na kuzuia mitandaoni taarifa za mtu binafsi ambazo zilirekodiwa kihalali na kusambazwa, kuwekwa wazi.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushauri wa hali ya faragha na usalama wa mawasiliano.

Kauli hiyo ya THRDC imekuja zikiwa siku chache baada ya Mbunge wa Ubungo (Chadema), Saeed Kubenea, kutaka TCRA kuwachukulia hatua wanaohusika na vitendo hivyo vya udukuzi.

Kubenea alisema hayo baada ya kudaiwa kuwa mawasiliano Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye na makatibu wakuu wastaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba, yamedukuliwa na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Jambo hilo lilibuka baada ya Kinana na Makamba kumwandikia barua Katibu wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu wa CCM, Pius Msekwa, wakilalamikia kile walichodai kuwa wamedhalilishwa na mwanaharakati Cyprian Musiba.

Olengurumwa alisema serikali inapaswa kutunga sheria hiyo ili kuepusha ukiukwaji wa haki ya faragha itakayoendana na Katiba ya Tanzania na mikataba mingine ya kimataifa kuhusu haki ya faragha na mawasiliano.

"Lipo tatizo kubwa sana kuhusu udukuzi na uingiliaji usio rasmi wa mawasiliano ya watu nchini Tanzania na wakati mwingine taratibu za kimahakama hazifuatwi hasa pale taarifa zinapohitajika kwa ajili ya mahitaji yaliyoainishwa kisheria," alisema.

INAENDELEA UK. 8

# Afariki akichimba udongo wa kujengea

**Na Shaban Njia,**
SHINYANGA

MKAZI wa kijiji cha Nyambui Kata ya Tinde wilayani Shinyanga, Hassan Tundu (26), amefariki dunia papo hapo baada ya kuangukiwa na kifusi wakati akichimba udongo kwa ajili ya kujenga nyumba.

Kamanda wa Pilisi Mkoa wa shinyanga, Richard Abwao, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Ijumaa iliyopita majira ya saa 11:00 jioni katika kitongoji cha Ngaka.

Abwao alisema chanzo cha tukio hilo ni kwa Tundu kuangukiwa na kifusi cha udongo akiwa na wenzake wawili.

Kwa mujibu wa Kamanda Abwao, mbali na Tundu kupoteza maisha, wenzake aliowataja kuwa ni Mihambo Mjiga (20) na Elias Magwala (26) waliokuwa wakichimba udongo huo, walijeruhiwa.

Abwao alisema mwili wa marehemu umekabidhiwa kwa ndugu kwa taratibu za mazishi baada ya uchunguzi wa madaktari kukamilika na kuongeza kuwa majeruhi walikuwa wanaendelea na matibabu katika Kituo cha


## KUMBUKUMBU



115341402

HOWARD SIMON MWANSASU

Leo tarehe 29th Julai, 2019 tunaadhimisha mwaka mmoja tangu ulipotutoka. Tunakupenda na tunaendelea kukumbuka mpendwa Baba yetu. Majonzi katika mioyo yetu ni makubwa sana na hayataweza kufutika. Pengo lako halitaweza kuzibwa na kitu chochote. Unakumbukwa sana na mkeo, watoto wako wa kike na kiume, wadogo zako, dada zako,wajukuu, ndugu, majirani na marafiki kwa ujumla.

*Mwenyezi Mungu aiweke roho yako mahali pema peponi. Amen.*


# Sugu alia polisi kuzuia mikutano

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Mbeya Mjini (Chadema), Joseph Mbilinyi, amelalmikia Jeshi la Polisi kwa kile alichodai kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara katika jimbo lake, kitendo alichokiita cha hujuma za kisiasa.

Katika kipande cha video kilichosambaa katika mitandao ya kijamii, mbunge huyo analilalamikia Jeshi la Polisi Mbeya kumzuia kufanya mikutano ya hadhara na wananchi wa jimbo hilo.

"Nimempigia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (Kangi Lugola) akasema nitakurudia, narudia tena nimempigia IGP (Simon) Sirro yeye mwenyewe anashangaa na kwa kurudia maneno yake akaniambia kwa nini polisi wa Mbeya wanazuia mikutano ya mbunge wakati Rais amesema wabunge wafanye mikutano kwenye maeneo yao," alisema. Gazeti hili lilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, kuhusu madai hayo na kukanusha huku akisema ni kutafuta umaarufu wa kisiasa na kwamba jeshi hilo halijazuia mikutano yake.

"Mikutano anafanya hata hivi karibuni amekuja Mbowe hapa na wamefanya mkutano. Aache kutafuta 'kick' za ajabu. Ni uongo mtupu. Mimi mwenyewe nampigia simu hapokei na nina ushahidi," alisema Kamanda Matei.

Nipashe ilimtafuta mbunge huyo kuhusu alichosema Kamanda Matei na kusema mikutano anayoifanya ni ya ndani na si mikutano ya hadhara na wananchi wake.

"Mikutano anayozungumzia ni mikutano ya ndani. Mimi nimezuiwa kufanya mikutano ya hadhara, wanataka kuwaaminisha mabosi wao kuwa Sugu kashapotea katika ramani, sasa tukifanya mkutano tutapiga nyomi (watu wengi) ya kutosha na tutawaumbua," alisema.

"Wamekuwa wakinitaka nikaombe ruhusa kwa mtendaji kinyume kabisa na utaratibu lakini huwa natii. Ukienda kwa mtendaji unakuta kaishapewa maagizo ya kuuzuia mkutano wangu," aliongeza.

Gazeti hili liliziona barua zilizojibiwa na Jeshi la Polisi kuhusu mbunge huyo kufanya mikutano katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo kama alivyoomba, zikitolewa sababu mbalimbali za kuzia mikutano hiyo.

"Mkabala na stendi ya Chunya mahali hapa ni barabarani na kwa ukubwa wa mkutano wa mbunge ambao unakuwa na watu wengi eneo hilo ni hatarishi kama gari litakosa breki linaweza kuleta madhara makubwa kwa wananchi watakaokuwapo kwenye mkutano," ilisema sehemu ya barua hiyo.

"Soko la Iganjo kata ya Iganjo eneo hapo sokoni halijaainishwa ni wapi mahususi pa kufanyia mkutano huo," ilieleza barua hiyo.

Akizungumza katika ziara yake ya kikazi mkoani Tabora hivi karibuni, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, alisema Rais John Magufuli alisharuhusu wabunge wafanye mikutano kwenye majimbo yao kwa sharti la kutoa taarifa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

## HABARI KITAIFA

# Lugola amtumbua mkuu wa usalama barabarani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemvua madaraka Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, Charles Bukombe, kwa madai ya kuyapuuza maagizo yake na kuyaita ya kisiasa.

Licha ya kumwondoa katika nafasi hiyo, Waziri Lugola amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, kumchukulia hatua za kinidhamu ili iwe fundisho kwa maofisa wa jeshi hilo na taasisi zingine chini ya wizara yake.

Lugola amesema ameshuhudia ofisa huyo katika video ambayo ilikuwa inasambaa mitandaoni akiwa katika mkutano jijini Arusha, akipinga maagizo yake na kuyaita ya kisiasa na kutoyatekeleza.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara wa wananchi wa Mji wa Malinyi, mkoani Morogoro jana, Lugola alisema yeye hatoi maagizo ya kisiasa bali yale yatakayomsaidia Rais (John Magufuli) kazi zake kwa wananchi wanyonge wanaopambana na umaskini na ajira.

"Namwagiza Katibu Mkuu achukue hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kumwondoa u-RTO (ukuu wa usalama barabarani mkoa) afanye shughuli zingine za kipolisi. Pia ma-RTO ambao mkono wangu haujafika kwenu na wengine nimeanza kuwaona hamsimamii vizuri maagizo yangu. Wako ambao wanaendelea na uonevu, pia wako baadhi ya askari wanaendelea kuchukua rushwa barabarani," alisema Lugola.

Pia Waziri Lugola aliwaonya wakuu wa usalama barabarani wa mikoa ya Morogoro na Mara akiwataka wajitathimini katika utendaji wao kabla hajawachukulia hatua.

"Wapo baadhi ya askari wanaonevu, wanaendelea kuchukua rushwa. Wajitathimini katika utendaji wao kabla sijawachukulia hatua kali za kinidhamu," alisema.

Lugola katika hotuba zake kwenye mikutano mbalimbali alisema serikali ya awamu ya tano ni sikivu na haitaki kumnyanyasa mwananchi yeyote kupitia makosa ya trafiki wasiokuwa waaminifu.

Lugola alitoa maagizo kwa Jeshi la Polisi nchini kuwa bodaboda zinazotakiwa kuwapo kituo cha polisi ni zile zilizoko katika makundi matatu ambayo ni ya kuhusika kwenye uhalifu, zilizotelekezwa au zilizookotwa na zilizohusika katika ajali.

"Bodaboda hizo ndizo zinapaswa kuwapo vituoni lakini kuziweka bodaboda ambazo hazipo katika makundi hayo, napiga marufuku na hii nataka polisi nchi nzima mnielewe," alisema Lugola.

Pia Lugola aliwataka waendesha bodaboda mjini Malinyi na Tanzania kwa ujumla wafuate sheria za usalama barabarani ikiwamo kuvaa kofia ngumu, kutokubeba abiria zaidi ya mmoja na kuwasha taa wakati wakiendesha.

Sambamba na hilo, Lugola alipiga marufuku tabia ya baadhi ya polisi nchini kukamata pikipiki wakiwa hawana sare na kwamba hilo limesababisha kero kwa madereva na anayekamatwa anaweza akadhaniwa kuwa ni jambazi.

# ACT-Wazalendo yatamba kunyakua majimbo Ilala

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama chao kimejiandaa kushinda kwenye uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Amesema chama hicho kitaongoza kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na kutoa wabunge wengi katika majimbo yote yaliyopo katika wilaya hiyo.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua matawi 10 ya chama hicho yaliyopo katika Kata ya Vingunguti, Jimbo la Segerea.

"Chama cha ACT-Wazalendo kimejipanga kushinda katika Wilaya ya Ilala, tunatoa wito kwa Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, ahakikishe kwamba uchaguzi wa serikali za mitaa unafanyika kwa uhuru na haki. Tunataka wananchi wakachague viongozi wanaowataka na siyo kuvuruga uchaguzi," alisema Zitto.

Kwenye uzinduzi wa matawi hayo, Zitto aliambatana na viongozi wengine wa ACT akiwamo Mshauri wa Chama, Maalim Seif Sharif Hamad na Katibu Mkuu wa chama, Dorothy Semu.

Kwa upande wake, Maalim Seif aliwataka vijana kusimama imara katika kutetea demokrasia hapa nchini kwa sababu wao ndiyo nguvu kazi ya taifa na wanaweza kuleta mabadiliko wanayoyataka.

Pia, aliwataka vijana kufikiria kesho yao kwa kuleta mabadiliko chanya ambayo yataleta maendeleo katika taifa kwa kuwataka kuwa wajasiri na kupigania demokrasia na maendeleo ya nchi yao.

Alisema ACT- Wazalendo ndiyo chama kinachobeba mahitaji ya wananchi na kuongoza nchi.

Zitto aliongoza ziara ya wanachama na viongozi wa chama hicho kuzindua matawi yao katika kata ya Vingunguti kwa kutembelea mtaa kwa mtaa na kufungua matawi mapya.



# TANGAZO

## International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 30.6.2019 | 31.03.2019 |
| A. | ***MALI*** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,667 | 3,688 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 25,172 | 19,508 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 15,041 | 9,138 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 11,761 | 19,894 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 418 | 452 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 52,068 | 53,465 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,080 | 3,165 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 677 | 699 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **110,883** | **110,008** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 8,056 | 9,025 |
| 18 | Amana za Wateja | 80,409 | 75,880 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 434 | 2,847 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 15 | 33 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,018 | 1,029 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 61 | 61 |
| 27 | Dhima Nyingine | 588 | 572 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | ***JUMLA YA DHIMA*** | **90,581** | **89,446** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **20,302** | **20,562** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,025 | 20,025 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,940 | 2,841 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (1,924) | (1,825) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (739) | (479) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **20,302** | **20,562** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 14,222 | 16,696 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,968 | 6,112 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,549 | 1,506 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 18% | 19% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13% | 11% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 60% | 63% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 48% | 50% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 71% | 75% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1% | -4% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1% | -2% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO LINGANISHI YA MWAKA ULIOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2019 | 30.06.2018 | 30.06.2019 | 30.06.2018 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,860 | 2,242 | 3,558 | 4,622 |
| 2 | Gharama za Riba | 814 | 853 | 1,654 | 1,996 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***1,046*** | ***1,389*** | ***1,904*** | **2,626** |
| | | | | | - |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 158 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 60 | 206 | 60 | 36 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | ***302*** | ***460*** | ***502*** | **905** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 72 | 77 | (7) | 102 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 39 | 233 | 97 | 72 |
| | 6.3 Gawio | | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 192 | 150 | 412 | 731 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | ***1,548*** | ***1,528*** | ***3,055*** | **3,103** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 551 | 648 | 1,188 | 1,241 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 66 | 63 | 133 | 79 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 930 | 818 | 1,734 | 1,783 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(259)** | **115** | **(709)** | 236 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | 30 | 30 | 60 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | ***(259)*** | ***85*** | ***(739)*** | 176 |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | ***(259)*** | ***85*** | ***(739)*** | **176** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 65 | 68 | 65 | 68 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (13) | 4 | (37) | 9 |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (13) | 4 | (37) | 9 |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -0.23% | 0.32% | -0.64% | 0.33% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -1.27% | 1.53% | -3.62% | 1.58% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 71.57% | 56.56% | 75.24% | 56.13% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 1.44% | 2.39% | 2.62% | 4.52% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA 30.06.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (259) | (449) | (709) | 236 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 241 | 89 | 330 | 472 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,336 | (168) | 1,168 | (4,153) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,148 | (3,408) | (2,261) | 10,685 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (13) | 1,125 | 1,112 | (707) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (541) | (2,036) | (2,577) | (1,166) |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | (30) | (30) | (60) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 653 | (1,964) | (1,311) | (2,403) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **2,565** | **(6,843)** | **(4,278)** | **2,904** |
| | | | | - | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (40) | (4) | (44) | (201) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (7,737) | (2,997) | (10,734) | 6,342 |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(7,778)** | **(3,001)** | **(10,779)** | **6,141** |
| | | | | - | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | - | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | - | - | - | - |
| | | | | - | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | - | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(5,213)** | **(9,844)** | **(15,057)** | **9,045** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 38,218 | 48,062 | 48,062 | 40,782 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **33,005** | **38,218** | **33,005** | **49,827** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **20,025** | **-** | **(1,825)** | **2,445** | **396** | **-** | **21,041** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (739) | | | | **(739)** |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | -99 | 122 | (23) | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.06.2019** | **20,025** | **-** | **(2,663)** | **2,567** | **373** | **-** | **20,302** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **20,025** | **-** | **(1,487)** | **3,132** | **464** | **9** | **22,143** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | 176 | | | | 176 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | - |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | | | | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.06.2018** | **20,025** | **-** | **(1,311)** | **3,132** | **464** | **9** | **22,319** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Saini:

**RAMA KRISHNA MARAKANI**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 26 JULAI 2019

**AMANI MWIDETE**
Mkuu wa fedha
Tarehe: 26 JULAI 2019

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 26 JULAI 2019

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

Saini:

**LIM TEONG LIAT**
Mwenyekiti wa Bodi
Tarehe: 26 JULAI 2019

**CHARLES RWECHUNGURA**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 JULAI 2019

# Watalii waliingizia taifa tril. 5/-

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka kufikia milioni 1.5 kutoka milioni 1.3 kwa mwaka 2017/18 huku wakiliingizia taifa Dola za Marekani bilioni 2.4 (sawa Sh. tril. 4.5).

Pia utalii wa wanyamapori ukiendelea kuwa kitovu cha kivutio na hivyo kuifanya sekta hiyo kuongoza kuchangia pato la taifa.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati akitoa taarifa ya takwimu za utalii na kwamba ukuaji huo ni mara mbili ya watalii wanaofanya utalii duniani.

Alisema katika mwaka 2018, wizara hiyo kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar na Idara ya Uhamiaji, ilifanya utafiti wa watalii wanaoondoka nchini kwa lengo la kupata taarifa zitakazosaidia kuandaa akaunti za taifa na takwimu za mizania ya malipo ya nje.

Alisema pamoja na kuongezeka kwa watalii, mapato yatokanayo na utalii yaliongezeka kwa asilimia 7.2 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.4 kutoka bilioni 2.3 zilizopatikana mwaka 2017.

Profesa Mkenda alisema masoko makubwa 15 yalichukua asilimia 71.8 yakiongozwa na Marekani ambayo ilikuwa ni asilimia 15.6 ikifuatiwa na Kenya na Uingereza.

Alisema wastani wa matumizi ya mtalii kwa siku nchini uliongezeka hadi Dola za Marekani 193.0 kutoka Dola 162.0 mwaka 2017, watalii walionunua huduma kwa vifurushi walitumia wastani wa Dola 331.0 kwa siku na wale ambao hawakununua huduma kwa mfumo huo walitumia wastani wa Dola 135.0.

Alisema watalii waliokuja kwa ajili ya likizo na burudani walikuwa asilimia 62.6 na wameendelea kuwa na wastani mkubwa wa matumizi wa Dola 394.0 kwa siku.

Alisema watalii walionunua huduma kwa vifurushi walitumia wastani wa Dola 465.0 kwa siku na wasiotumia mfumo huo walitumia wastani wa Dola 162.0

Profesa Mkenda alisema watalii waliotembelea Tanzania walikaa kwa wastani wa siku 10 katika mwaka 2018, waliokuja kutembelea ndugu na jamaa walikaa kwa wastani wa siku 11.



"Utalii wa wanyamapori umeendelea kuwa kitovu cha kivutio nchini kwa sababu Tanzania ina hifadhi za wanyama na mapori ya akiba mengi," alisema Profesa Mkenda na kuongeza kuwa utangazaji pamoja na miundombinu bora iliyopo kwenye vivutio hivyo imechangia utalii wa wanyamapori kushamiri.

Hata hivyo, Profesa Mkenda, alisema serikali inatarajia kuongeza matangazo ili kuvutia zaidi watalii na kufikia idadi ya watalii milioni tano kwa mwaka kama ambavyo Rais John Magufuli alivyoagiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa NBS, Albina Chuwa, alisema takwimu hizo za watalii zitasaidia kuboresha sekta hiyo na kufanya uchambuzi wa kina kuimarisha sekta hiyo.

Alisema kupitia takwimu hizo itasaidia kuweka mipango ya kukusanya mapato zaidi na kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali.

Kamishna wa Uhamiaji, Idara ya Vibali, Mary Palmer, alisema wamekuwa wakisimamia mlolongo mzima na kuhakikisha mgeni anapata huduma jambo linaloboresha sekta hiyo.

# NSSF yasajili wanachama wapya 472

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limeandikisha wanachama wapya 472 kwenye sekta binafsi na sekta isiyo rasmi kupitia kampeni ya 'NSSF na Marafiki' iliyoanzishwa mwishoni mwa wiki.

Meneja Kiongozi Uendeshaji wa NSSF, Cosmas Sasi, aliyasema hayo alipotembelea kampuni ya KK Security Mkoa wa Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Alisema kupitia kampeni hiyo, NSSF itapita kwa kila mwajiri ili kuhakikisha wanasajili wafanyakazi wao na kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa wakati.

"Tumezindua kampeni maalumu inayoitwa 'NSSF na Marafiki'. Kupitia kampeni hii, tunapita kwa waajiri wote Tanzania nzima kuhakikisha waajiriwa wote wanaandikishwa. Kampeni hii ni ya kirafiki ambayo waajiri sasa wanashirikiana na NSSF kuhakikisha wafanyakazi wao wanaandikishwa kwenye mfuko ikiwa ni takwa la kisheria," alisema Sasi.

Meneja wa NSSF Mkoa wa Kinondoni, Hiza Kiluwasha, alisema dhana ya kampeni hiyo ni kuwapatia elimu wanachama kuhusu umuhimu wa kujiunga na kuchangia NSSF.

"Kampeni yetu mpya kabisa sasa hivi ni NSSF na marafiki kwa hiyo marafiki wetu ni wanachama wa NSSF na waajiri, sasa kuhakikisha rafiki yako lazima uwe unamtembelea kila wakati pia kwa marafiki zetu wote ambao bado hatujawafikia kwa kuzingatia kampeni hii basi waje katika ofisi zetu za NSSF kwa ajili ya kujiandikisha au kupiga simu " alisema.

Naye Mwakilishi wa Idara ya Rasilimali Watu wa KK Security, Victor Gaudence, alishukuru NSSF kwa kuwatembelea na kutoa elimu ya hifadhi ya jamii iliyofanikisha kusajili wafanyakazi 472 wa kampuni hiyo.

Kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, NSSF inatoa huduma ya hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, hivyo kampeni hiyo itasaidia kuongeza wanachama kutoka katika sekta hizo

International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014

MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES- As at 30th June 2019

| PRODUCT TYPE | TZS | USD | GBP | EUR |
|---|---|---|---|---|
| **SERVICES** | | | | |
| Monthly Statement Current Accounts | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement Savings Accounts | Free | Free | Free | Free |
| E-statement | Free | Free | Free | Free |
| Interim statement - per page | 1,000 | 1 | 1 | 1 |
| **MINIMUM ACCOUNT OPENING** | | | | |
| Savings Account-Salaried | Free | Free | Free | Free |
| Savings Account-Normal | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| Current account-Normal | 50,000 | 100 | 100 | 100 |
| Current account -Premium | 1,000,000 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| **CASH WITHDRAWALS OVER THE COUNTER** | | | | |
| Savings account - A | | | | |
| I. Above 500,000 | Free | NA | NA | NA |
| II. Less than 500,000 | 1,000 | NA | NA | NA |
| Savings account - B | | | | |
| I. Up to USD/GBP 10,000 | NA | 5 | 5 | 5 |
| II. Above USD/GBP 10,000 | NA | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| | | | | |
| Current account | | | | |
| I. Up to 5,000,000 | Free | NA | NA | NA |
| II. Above 5,000,000 | 2,000 | NA | NA | NA |
| Current account | | | | |
| I. Up to USD/GBP 10,000 | NA | 5 | 5 | 5 |
| II. Above USD/GBP 10,000 | NA | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| Third Part withdraw per leaf | 30,000 | 30 | 30 | 30 |
| **CASH HANDLING FEE** | | | | |
| Deposits on Small Denominations Less than $50 | 3% | 3% | 3% | 3% |
| | | | | |
| **ATM WITHDRAWALS** | | | | |
| On Us | 600 | NA | NA | NA |
| On Others | NA | NA | NA | NA |
| **OTHER ATM TRANSACTIONS** | | | | |
| Issue of ATM Card(New) | 6,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card (faulty) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card (worn out) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Replacement ATM Card(Lost) | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| **TRANSFERS** | | | | |
| Internal transfers | Free | Free | Free | Free |
| Interbranch Transfer | Free | Free | Free | Free |
| **STANDING ORDERS** | | | | |
| Standing orders (within bank) | 1,500 | 0.50 | 0.50 | 0.50 |
| Standing orders (to other banks Local Currency ) | 11,800 | NA | NA | NA |
| Standing orders (to other banks ) below usd 10,000 | NA | 3 | 3 | 3 |
| Standing orders (to other banks ) above usd 10,000 | NA | 10 | 10 | 10 |
| Unpaid standing orders | 40,000 | 20 | 20 | 20 |
| **CHEQUES** | | | | |
| Cheque book issuance | | | | |
| I. Personal chq book with 25 leaves | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| II.Corporate chq book with 50 leaves | 50,000 | 20 | 20 | 20 |
| III.Corporate chq book with 100 leaves | 70,000 | 35 | 35 | 35 |
| Counter cheque charges per leaf | 20,000 | 20 | 20 | 20 |
| Stop Payment orders -per instructions/ Cheque series | 40,000 | 20 | N/A | N/A |
| **Outward Cheque Unpaid (Chq returned by Us)** | | | | |
| I. Refer to Drawer | 50,000 | 50 | N/A | N/A |
| II. Effect not Cleared | 30,000 | 30 | N/A | N/A |
| III. Any Technical reason (Like endorsement) | 10,000 | 5 | N/A | N/A |
| **Inward Cheque Unpaid (Chq returned by other bank)** | 10,000 | 5 | N/A | N/A |
| Inward Cheques processing per leaf | 500 | 1 | N/A | N/A |
| | | | | |
| Bankers Cheque (account holders) | 15,000 | 10 | N/A | N/A |
| Re- Purchase of Bankers cheque on customers request | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Uncollected Cheque book (after one Month) | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| **OTHER SERVICES** | | | | |
| Current Account Closure on customer's request | 30,000 | 15 | 15 | 15 |
| Savings Account Closure on customer's request | 20,000 | 5 | 5 | 5 |
| Cheque Force clearance (with one day float) | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Chq Force clearance (with more than one day float) | 40,000 | 20 | 20 | 20 |
| Dormant Charges for Savings account | Free | Free | Free | free |
| Dormant Charges for current account | 25,000 | 15 | 15 | 15 |
| Dormant account Activations | Free | Free | Free | free |
| Account Maintanance Charge - Savings | 1,000 | 2.50 | 2.50 | 2.50 |
| Account Maintanance Charge - Current | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| Certificate of balance | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Letter of introduction | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Salary handling | Free | Free | Free | free |
| School fees deposits | Free | Free | Free | Free |
| Un arranged Temporary Overdrafts (TODs) | 24% | 10% | 10% | 10% |
| Corporate Premier Account Maintanance Charge | 20,000 | 20 | N/A | N/A |
| Individual Premier Account Maintanance Charge | 20,000 | 20 | N/A | N/A |
| Lost Cheque charges | 20,000 | 18 | 18 | 18 |
| EFT charges: | | | | |
| On Us | 300 | Free | N/A | N/A |
| On Others | 11,800 | NA | N/A | N/A |
| **TRADE FINANCE** | | | | |
| **Remittance** | | | | |
| Demand draft | NA | NA | NA | NA |
| Outward Local transfers ( TISS) | 11,800 | 11.80 | NA | NA |
| Outward Foregin transfers -Up to USD50,000 | NA | 50 | 50 | 50 |
| Outward Foregin transfers - above USD50,000 | NA | 75 | 75 | 75 |
| Inward Local transfer (TISS) | Free | Free | Free | Free |
| Inward Foreign transfer | NA | 15 | 15 | 15 |
| **Bonds & Guarantees** | | | | |
| Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Extentions | 1.42% Per Quarter | | | |
| Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| Cancellations of guarantees if not Returned | 20,000 | | | |
| **Advance Payment Guarantees** | | | | |
| Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance swift charges | Usd 50 | | | |
| **Export Collections (EC)-Outwar Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance Commission-per tracer | Usd 50 | | | |
| Courier Charges | Usd 100 | | | |
| **LOAN & ADVANCES** | | | | |
| Loan Processing Fees | 1.82% | | | |
| Early Loan Repayment Charges | 1% | | | |
| | | | | |
| **BASIC LENDING RATE** | 24% | 10% | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

Ramakrishna Marakani — Chief Executive Officer — 26.07.2019

Christome Tembo — Head of Operation — 26.07.2019

John Mwakasonda — Head of Internal Audit — 26.07.2019

## MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# *Wachezaji wazawa Ligi Kuu watakiwa kubadilika*

**ZIKIWA** zimebakia siku 25 kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa 2019/20 ili Ligi Kuu Tanzania Bara iweze kuanza, kumekuwa na mijadala mbalimbali kuhusiana na idadi ya wachezaji wa kigeni ambao wanatakiwa kuruhusiwa kusajiliwa.

Ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, itaanza Agosti 23 na mabingwa Simba wataanza kampeni ya kutetea taji hilo kwa kuwavaa JKT Tanzania, wakati Yanga yenyewe itakutana na Ruvu Shooting.

Hata hivyo, kabla ya pazia hilo la Ligi Kuu Tanzania Bara halijafunguliwa rasmi, Simba inayonolewa na Mbelgiji Patrick Aussems, itavaana na Azam FC katika mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii, utakaochezwa Agosti 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Hii ndio inaleta maana kwamba, mchezaji wa kigeni ambaye atasajiliwa na timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara, anatakiwa kuwa na kiwango cha juu katika nafasi yake ukilinganisha na wachezaji wengine wa nafasi hiyo ambao amewakuta kwenye timu husika. Kanuni pia inaeleza kuwa ni lazima mchezaji wa kimataifa atakayesajiliwa anatakiwa awe ametoka kwenye ligi ya juu na vile vile awe pia ni nyota aliye kwenye kikosi cha taifa lake.

Hii inalenga kuzuia wachezaji kutoka mataifa mengine kuja "kujaribu bahati" na kuziba nafasi za wachezaji wazawa, ambao wanaweza kupoteza fursa hiyo kwa kuzidiwa na ukubwa wa jina la nchi anayotoka mchezaji huyo wa kimataifa.

Ili taifa lolote liweze kufanya vema katika mashindano mbalimbali inayoshiriki, ni lazima litengeneze mfumo sahihi ambao utawajenga na kuwaimarisha wachezaji wake.

Na kwa hapa nchini, Ligi Kuu Tanzania Bara, ndiyo inayozalisha wachezaji wengi wanaoitumikia Taifa Stars ambayo kwa sasa inawania nafasi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Kwa kuzingatia hili, ndio maana Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), serikali na wadau mbalimbali wa mchezo huo unaopendwa zaidi, wamekuwa wakitoa mawazo yenye malengo ya kujenga kuhusu wachezaji wa kimataifa wanaotakiwa kusajiliwa.

Nipashe linawataka wachezaji wazawa kuhakikisha wanajituma na kucheza katika kiwango cha juu ili kuwafanya watunga sera wasione sababu ya kuruhusu idadi kubwa ya nyota wa kigeni kusajiliwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na timu moja.

Endapo wachezaji wazawa, wataonyesha bidii, watawafanya viongozi wa timu za hapa nchini kuacha kufikiria kusajili wageni, na vile vile hali hii itapelekea Taifa Stars kufanya vema katika michuano mbalimbali itakayoshiriki.

Ni jambo lisilopingika kuwa, Taifa Stars inategemea wachezaji wengi kutoka kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, idadi ambayo ilijidhihiridha ilipokuwa na nyota wengi katika kikosi kilichoshiriki fainali zilizopita za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019).

Tunapenda kuwakumbusha wachezaji wazawa kuwa, mbali na kuisadia Taifa Stars kupeperusha vema bendera yake, vile vile itawafanya wapate kipato kizuri kwa kusajiliwa kwa kiwango kikubwa cha fedha, sambamba na kulipwa mishahara minono.

Mpira Pesa, hii kauli ili iweze kutimia kwa wachezaji wetu wa Kitanzania kama ambavyo tumeshuhudia nyota Mganda Emmanuel Okwi, alivyokataa mamilioni ya Simba na kwenda kujaribu maisha kwingine, ni wakati wa wachezaji wetu kupandisha viwango vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# *Kaseja karudi Stars, Yosso mnakosea wapi?*

**BAADA** ya miaka sita kupita, hatimaye 'Tanzania One' wa zamani nchini, Juma Kaseja amerejea kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Na jana amedaka kwenye mechi ambayo Stars imecheza dhidi ya Kenya (Harambee Stars), katika mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Kurejea kwa Kaseja kwa mara nyingine tena kwenye kikosi cha Stars kumewashangaza mashabiki wengi wa soka. Wanashangazwa kwa kipa mkongwe kama Kaseja ambaye alikuwa tayari taratibu ameshaanza kuwa kocha wa makipa, kabla ya kwenda kwenye soka la ufukweni.

Lakini ghafla akarejea kwa kasi akiwa na klabu ya KMC na kuiwezesha kushika nafasi ya nne, ikiiwezesha kutinga kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hakuna ambaye haujui uwezo wa Kaseja. Kuna wakati aliitwa 'Tanzania One'. Aliwahi kuwaliza Zamalek nchini Misri alipopambana akiwa kwenye milingoti mitatu hadi kufanya mechi ya Ligi ya Mabingwa kwenda kwenye hatua ya mikwaju ya penalti mwaka 2003. Alipangua penalti mbili na kuiwezesha Simba kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa, ikiivua ubingwa Zamalek.

Mshangao wa wengi ni kwamba baada ya miaka mingi kurejeshwa tena Taifa Stars, ikitegemewa kuwa uwezo wake utakuwa umeshuka na sasa kutakuwa na vijana wengi waliochipukia watachukua nafasi yake.

Alijiunga na Simba mwaka 2002 akitokea Moro United ya mkoani Morogoro. Fikiria tangu mwaka huo hadi sasa ni miaka 17. Amerejea tena kwenye timu ya taifa.

Kijana aliyekuwa na mwaka mmoja wakati huo kwa sasa atakuwa na miaka 17 sasa. Kaseja bado yupo golini. Sababu ni nini?

Kwanza kabisa Kaseja ni mpenzi wa mazoezi. Anapenda kufanya sana mazoezi na hii inamweka fiti siku zote.

Kingine ni kwamba Kaseja hana mambo mengi nje ya uwanja. Ni mtu anayejitunza mno na hawajawahi kuwa na historia ya utovu wa nidhamu hasa akiwa nje ya uwanja.

> **Pamoja na kwamba kuna dhana kuwa makipa wanakaa kwenye soka kwa muda mrefu, lakini hapa Tanzania wengi wanakaa kwa muda mfupi na hata wanaokaa kwa muda mrefu hawawi kwenye kiwango cha juu kwa muda mrefu pia.**

Pamoja na kwamba kuna dhana kuwa makipa wanakaa kwenye soka kwa muda mrefu, lakini hapa Tanzania wengi wanakaa kwa muda mfupi na hata wanaokaa kwa muda mrefu hawawi kwenye kiwango cha juu kwa muda mrefu pia. Jambo lingine la muhimu ni kwamba makipa wengi wa sasa Tanzania hawana viwango vya hali ya juu kama wale wa zamani.

Ukiondoa Aishi Manula, Benno Kakolanya na kidogo kwa sasa Metacha Mnacha na Aron Kalambo, wengine wote ni wa kawaida tu.

Nina uhakika kuwa Kaseja wa mwaka 2003 aliyeipeleka Simba kwenye makundi Ligi ya Mabingwa siyo huyu wa sasa. Lakini kwa aina ya makipa tulionao Tanzania leo, Kaseja bado anaonekana ana uwezo mkubwa kwa sababu si wengi wenye uwezo wa kumpita yeye, au kuwa kama yeye zaidi ya hao wanne tu niliowaainisha.

Zamani Tanzania ilikuwa na makipa wengi mahiri, waliokuwa wakicheza kwa muda mrefu kiasi cha hata kocha wa timu ya taifa kuumiza kichwa.

Makipa vijana wa sasa inapaswa wajiulize wanakosea wapi? Hivi wanajisikiaje kama wao makipa vijana kabisa wanaodaka kwenye klabu mbalimbali za Ligi Kuu wameachwa na kurejeshwa kipa mkongwe? Kama ni kipaji wao nao si wanavyo?

Tatizo ni lile, kujituma na nidhamu. Kuanzia sasa wanapaswa walifanyie kazi suala hili, vinginevyo Kaseja anaweza kurejea tena kuwa 'Tanzania One' na wao wakiwa hapo hapo wanamuangalia.

Uwezo wao na kujituma ndiyo kutamfanya Kaseja atandike daluga. Kama anaona pamoja na ukongwe wake bado hawawezi kumfikia basi anaweza kukaa tena golini kwa miaka 10 tena ijayo.

Makipa vijana mnakosea wapi?

HABARI KITAIFA

# Waziri atoa matumaini bei ya umeme

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewahakikishia Watanzania kuwa serikali itashusha gharama za umeme ili kuwapunguzia mzigo wananchi wa hali ya chini na taasisi za elimu.

Dk. Kalemani alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi rasmi wa jina la Shule ya Sekondari ya Fountain Gate Academy iliyoko Miyuji, jijini hapa.

Alisema serikali inakusudia kupunguza gharama hizo pindi mradi mkubwa wa umeme katika Mto Rufiji, maarufu kama Strieglers Gorge, utakapokamilika.

"Hadi sasa katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, nchi yetu ndiyo inayotoza gharama za chini kwa yuniti moja tofauti na wengine na tutaendelea kupunguza," alisema.

Waziri kalemani alisema kwa gharama hizo, kutasaidia wananchi wa hali ya chini kumudu gharama za kuunganisha umeme na kulipia ankara za kila mwezi.

Aliongeza kuwa kupungua kwa gharama hizo kutapunguza malalamiko yanayojitokeza kwenye shule hasa za bweni ambazo wananfunzi wake hulazimika kujisomea nyakati za usiku.

Alitoa wito kwa wazazi kuunga mkono juhudi za watu wanaotoa huduma za elimu nchini kwa kuwahimiza watoto kupenda masomo pamoja na kulipa ada kwa wakati ili kuwezesha kuhudumia shule zao.

Dk. Kalemani aliwashauri wanafunzi kusoma kwa malengo huku akiutaka uongozi wa shule hiyo kutoa zawadi kwa walimu na wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shule za Fountain Gate Academy, Japhet Makau, alisema shule iliyozinduliwa jina jipya awali ilikuwa ikiitwa shule ya sekondari Azimio na ilikuwa inamilikiwa na mtu mwingine na menejimenti tofauti kabla ya kukabidhiwa kwao Mei, mwaka huu. Alibainisha kuwa kwa sasa shule hiyo itaitwa Fountain Gate Academy na wamebadilisha uongozi na mmiliki, hivyo wananchi watarajie mabadiliko makubwa katika elimu mkoani hapa.

Alisema baada ya serikali kutangaza kuhamishia makao makuu yake Dodoma, uongozi huo uliona umuhimu wa kupeleka huduma ya elimu katika eneo hilo kutokana na mahitaji makubwa.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, walianza na kufungua shule ya awali mwaka 2017 na 2018 walifungua shule ya msingi na mpaka sasa wana zaidi ya wanafunzi 1,000.

Makau alisema mpaka sasa shule hizo zinasomesha watoto wenye walemavu na yatima wapato 20 ambao wanahudumiwa kila kitu bure na wanaishi bweni.

# Udukuzi mawasiliano waibua wanaharakati

INATOKA UK. 2

Hivi karibuni sauti zinazodaiwa kuwa za viongozi wastaafu wa CCM, zilisambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii za kuzua taharuki, hali iliyosababisha watu mbalimbali kuwa na tafsiri tofauti kuhusiana na sauti hizo ingawa hakuna aliyejitokeza kukana au kuthibitisha ukweli wa sauti hizo.

Alisema kifungu cha 16 (I) cha Katiba ya Tanzania kinaeleza kuwa: "Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi."

Pia alisema THRDC inawataka watoa huduma za mawasiliano kuhakikisha wanalinda heshima ya biashara zao kwa kulinda taarifa za faragha za wateja wao na kwamba wananchi ambao haki zao za faragha zimevunjwa wanapaswa kwenda kufungua kesi mahakamani.

"Watu wote ambao haki yao ya faragha imevunjwa, wanahimizwa kufungua kesi katika Mahakama Kuu Kanda yoyote nchini, kuwashtaki watoa huduma au watu binafsi walioingilia kwa namna yoyote kudukua na kutumia mawasiliano hayo bila hati ya ruhusa ya mahakama," alisema Olengurumwa.

Alisema watu hao wanaweza kwenda kufungua kesi na kushtaki watoa huduma za mawasiliano kwa kuwa ni kosa kuvujisha mawasiliano ya mtu bila ya lidhaa.

Hivi karibuni, Mbunge wa Ubungo (Chadema), Saed Kubenea, aliibuka na kulaani vikali watu wanaoshiriki kuvujisha, kurekodi na kusambaza kwa watu taarifa za mitandao ya simu huku akisisitiza kuwa watu hao wanatakiwa kuchukuliwa hatua.

Kutokana na vitendo hivyo, Kubenea aliitaka Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), kujitathimini na kuacha kuruhusu kufanya udukuzi wa sauti za watu kama lilivyo sakata la viongozi mbalimbali wa CCM, wakiwamo wastaafu waliodaiwa kurekodiwa.

Amesema ni jambo la ajabu pale viongozi wanapofanya mazungumzo yao na kisha kuwekwa wazi kwa mfululizo wa mwendelezo wa mazungumzo hayo.

"Hii ni hatari sana kama viongozi wanafanywa hivi kwa mambo ya faragha kutolewa si hata baadaye watu wanaweza kuvunja ndoa za watu. Kama Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, amezungumza na hawara kwa mfano ikatoka nje si jambo la hatari hili.

Kuna vitu ambavyo vinatakiwa kuwa na usiri kwa maana kama hawa ni viongozi tu, je wananchi wa kawaida inakuaje," alihoji.

Msemaji wa TCRA, Semu Mwakyanjala, alipoulizwa baada ya Kubenea kutoa kauli hiyo, alisema mamlaka hiyo haihusiki na jambo hilo kwa kuwa ni la kijinai, hivyo linapaswa kushughulikiwa na vyombo vya dola husussan polisi.






# Yara yahakikishia wakulima pembejeo

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya mbolea ya Yara Tanzania imewahakikishia wakulima kupata pembejeo za kilimo ikiwamo mbolea kwa wakati na bei inayokubalika sokoni sambamba na msimu wa kilimo ili kuleta tija na kuongeza uzalishaji wa mazao nchini.

Akizungumza na mawakala na wasambazaji wa mbolea kutoka kanda zote nchini, Mkurugenzi wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema upatikanaji wa mbolea kwa wakati na bei nzuri kwa mkulima ma ni moja ya vipaumbele vya kampuni yake kuona uzalishaji wa mazao unaongezeka.

"Yara inaishukuru serikali kwa kuunga mkono juhudi zetu za kukuza na kuendeleza kilimo hapa nchini. Kama kampuni tumejipanga kuhakikisha mkulima anapata mbolea kwa wakati na matumizi bora ili kuleta tija katika uzalishaji," Odhiambo alisema.

Alisema kampuni imeshatoa elimu kwa mawakala na wasambazaji wote nchi nzima umuhimu wa kumfikishia mbolea mkulima kwa wakati na wakati huo maofisa ugani wamekuwa wakitoa mafunzo ya matumizi bora ya mbolea kwa wakulima.

Alisema Yara imejipanga vizuri katika msimu unaokuja wa kilimo kwa kuhakikisha mbolea inakuwapo wakati wote na mawakala na wasambazaji wanawajibika katika kuwafikishia huduma wakulima namna bora ya matumizi ya mbolea ili tija ya uzalishaji iweze kuongezeka.

"Wakati tunaelekea kuanza msimu wa kilimo mwezi ujao, tumetoa elimu kwa mawakala wetu na wasambazaji kabla hawajaanza kuuza mbolea kwa wakulima elimu kwanza ni muhimu sana katika kufanikisha kilimo bora na chenye tija," Odhiambo alisema.

Alisema lengo la kampuni ya Yara pamoja na kufanya biashara, imejikita zaidi katika kutoa elimu kwa wakulima umuhimu wa kupima afya ya udongo kabla ya kufanya kilimo.

Kupima afya ya udongo kutampa majibu mkulima kuhusu aina ya zao analotakiwa kupanda na aina ya mbolea anayopaswa kutumia na kwa kiwango gani kulingana na hali ya udongo wake hali itakayoongeza tija na uzalishaji wa mazao.



Wachuuzi wa machungwa sokoni Buguruni, wakisubiri wateja wa jumla na rejareja. Matunda hayo kwa sasa yanapatikana kwa wingi katika masoko mbalimbali ya Dar es Salaam huku baadhi yakiharibika kwa kukosa wateja. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ajali magari, bodaboda zaongezeka

**Na Mashaka Mgeta**

IDADI ya madereva wa magari na pikipiki waliopata ajali na kuorodheshwa katika Taasisi ya Mifupa (MOI) jijini Dar es Salaam, imeongezeka kwa asilimia 52.52 na asilimia 18.04 kwa kipindi cha kati ya 2017 na 2018.

Takwimu hiyo ni sehemu ya taarifa iliyopatikana MOI kwa waandishi wa habari wanaoshiriki mpango wa Alumnae wa usalama barabarani unaoratibiwa na Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF).

Kwa mujibu wa takwimu hizo, idadi ya madereva wa magari waliorekodiwa kupata ajali na kufikishwa MOI kwa mwaka 2018 walikuwa 754, ikiwa ni ongezeko la 396 kutoka 358 mwaka 2017.

Kwa upande wa madereva wa pikipiki, idadi yao kwa mwaka 2018 ilikuwa 1,813 wakati mwaka 2017, waliofikishwa MOI walikuwa 1,486.

Hata hivyo, takwimu kutoka kikosi cha usalama barabarani zinaonyesha katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 2009, ulevi umekuwa miongoni mwa vyanzo vya ajali.

Takwimu zilizotolewa na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Musilimu, zinaonyesha kuwa mwaka 2010 kulikuwa na kiwango kikubwa cha ulevi kurekodiwa kwa madereva, kilipofikia 580. Miaka mingine na kiwango chake kwenye mabano ni 2009 (221), 2011 (1717), 2012 (112), 2013 (91), 2014 (95), 2015 (66), 2016 (97), 2017 (93) na 2018 (61).

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa na Magonjwa ya Ajali wa MOI, Dk. Kennedy Nchimbi, alisema baada ya serikali kupiga vita matumizi ya pombe maarufu kama 'viroba' mwaka juzi, idadi ya ajali kwa madereva waliopata ajali na kufikishwa kwenye taasisi hiyo ilipungua.

Kauli ya Dk. Nchimbi inawiana na taarifa ya kitengo cha takwimu cha MOI inayoonyesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2016, madereva wa magari waliopata ajali na kufikishwa kwenye taasisi hiyo walikuwa 381 wakati wa pikipiki wakiwa 1,799.

"Kwa hiyo utaona kwamba baada ya 'viroba' kupigwa marufuku 2017, idadi ya madereva waliopata ajali ilishuka," alisema. Lakini takwimu za mwaka jana zinaonyesha kuwapo ongezeko hilo.

Hata hivyo, Dk. Nchimbi alisema madereva wanaopata ajali na kufikishwa MOI hawapimwi ili kuwabaini kama wametumia kilevi ama lah. "Wakati mwingine tunawasikia jamaa zao wanaowaleta wakielezea kwamba walewa, ama wakati mwingine kupitia harufu tu, tunabaini kwamba mhusika fulani alikuwa amekunywa kilevi na pengine ikachangia kupata ajali," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Nchimbi, sehemu kubwa ya madereva wanaosadikiwa kutumia kilevi wakati wa kuendesha magari na kupata ajali, wanabainika wakati wa mwisho wa juma hususani nyakati za usiku.

"Lakini hata kama akisaidikiwa kunuka pombe ama ndugu zake kuthibitisha kwamba dereva mhusika alitumia kilevi kabla ya kupata ajali, kitaaluma hatuandiki hivyo kwa maana itakuwa sawa na kumshutumu mgonjwa," alisema.

Sheria ya Usalama Barabarani inazuiwa matumizi ya kilevi kwa madereva, wakiruhusiwa kutovuka kipimo cha 0.008 cha kilevi kwenye damu (ABC) wakati Shirika la Afya Duniani (WHO) limeweka kiwango kama hicho kuwa ni 0.005 ABC.

Naye Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Musilimu, anasema marekebisho ya sheria ya usalama barabarani yapo katika hatua nzuri baada ya kupitishwa na kikao cha makatibu wakuu wa wizara.

"Ningependa sana kiwango hicho cha kilevi kiwe sifuri kwa hapa nchini, lakini kwa vile mwili wa binadamu una mmeng'enyo inayotengeneza kiwango kidogo cha kilevi mwilini, hatuna namna," anasema.

Kwa mujibu wa Kamanda Musilimu, ulevi kwa madereva ni miongoni mwa masuala muhimu yanayotajwa kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani.

# Raia Hungary adaiwa kukutwa dawa za kulevya gramu 250

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Hungary, Akos Berger (28), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na shtaka la kukutwa na dawa za kulevya aina ya Amphetamine yenye uzito wa gramu 250.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Gloria Mwenda, ulidai kuwa Julai 19, mwaka huu eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, alikutwa akisafirisha dawa.

Hakimu Kasonde alimtaka mshtakiwa kutokujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Mwenda alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu alisema mshtakiwa apelekwe mahabusu na kesi hiyo itatajwa Agosti 9, mwaka huu.

Wakati huo huo, wafanyabiashara wawili wakazi wa jijini Dar es Salaam walifikishwa katika mahakama hiyo wakikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya kilo 21.67.

Wakili wa Serikali, Daisy Makakala, aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Ramadhan Gumbo (25), mkazi wa Ilala na Fahad Salehe (24).

Makakala alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi kuwa Julai 13, mwaka huu, maeneo ya Mbezi wilayani Kinondoni, walisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride.

Hakimu Shaidi aliwataka washtakiwa kutojibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka.

Hata hivyo, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na Hakimu Shaidi aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 9, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wamerudishwa rumande.

# JNICC yafunguka mkutano wa SADC

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KUFANYIKA kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) ni heshima kubwa kwa Tanzania na Mwalimu Nyerere, miongoni mwa waasisi wa jumuiya hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Elishilia Kaaya, alisema taasisi yake imefurahishwa na uamuzi wa SADC kufanya mkutano kwenye kituo kilichopewa jina la Mwalimu Julius Nyerere ambaye ni miongoni mwa viongozi waliokuwa mstari wa mbele katika uanzishwaji wa jumuiya hiyo.

"Tunadhani SADC kuamua kufanya mkutano katika kituo chetu cha JNICC ni heshima kwa Tanzania na Mwalimu Nyerere hasa kutokana na mchango wake katika ukombozi wa nchi zilizo kusini mwa Afrika uliopelekea kuanzishwa kwa jumuiya hii," alisema.

Kaaya aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Muungano wa Tanzania na SADC kwa uamuzi huo ambao alisema umeipa nchi heshima na kuonyesha kwa vitendo namna ambavyo SADC inaheshimu mchango wa Tanzania katika uanzishwaji wa jumuiya hiyo.

Alisema kituo chake kinaendelea kufanya maandalizi ya msingi katika kituo chake kwa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha huduma zitakazohitajika zitolewa kwa viwango vya hali ya juu.

"Tunadhani sisi ni taasisi yenye uzoefu mkubwa katika kuhudumia mkutano ya kimataifa kama wa SADC na tuna timu ya watu wenye uzoefu katika kuhudumia wageni wa kimataifa kama kauli mbiu yetu inavyosema 'kuleta dunia Tanzania'," alitamba.

## Miaka mitano jela kwa wizi wa pikipiki

**Na Happy Severine,** MASWA

MAHAKAMA ya hakimu mkazi Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, imewahukumu wakazi wawili wilayani hapo kwenda jela kifungo cha miaka mitano kila mmoja kwa kosa la wizi wa pikipiki.

Waliohukumiwa ni Benjamin Lawalawa (19), mkazi wa Kijiji cha Lalago na John Paulo (31), mkazi wa mtaa wa Jashimba.

Mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Maswa, Tumain Marwa, Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi Mkaguzi Msaidizi wilayani hapo, Inspekta Rashidi Achimtole, aliiambia mahakama watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Oktoba 28, 2018, majira ya saa 11.30 jioni.

Mwendesha Mashtaka Inspekta Achimtole, aliiambia mahakama kuwa watuhumiwa wanatuhumiwa kwa kosa la wizi wa pikipiki yenye thamani ya Sh. milioni 2,100,000, mali ya Sitta Simon, mkazi wa Kijiji cha Lalago wilayani hapo.

"Siku ya tukio mtuhumiwa namba moja ambaye ni Benjamin Lawalawa aliendaa kuazima pikipiki ya mjomba wake ambaye ni Sitta Simoni, kwa ajili ya kuitumia na kuahidi kumwekea mafuta na baadaye atairejesha, mtuhumiwa hakuirudisha pikipiki hiyo na kutokomea nayo akiwa njiani kuelekea wilayani Maswa, ghafla mafuta yalimwishia na aliamua kuipeleka kwa mtuhumiwa namba mbili ambaye ni John Paulo," alidai.

"Mmliki wa pikipiki hiyo ambaye alipoona pikipiki yake haijarudishwa aliendaa kutoa taarifa katika kituo cha polisi wilayani Maswa," aliongeza.

Awali ilidaiwa kuwa mtuhumiwa Lawalawa alimuuzia Simon pikipiki hiyo na badaye alitoroka na pikipiki hiyo kwenda wilayani Igunga mkoani Tabora na jeshi la polisi wilayani Maswa kwa kushirikiana na jeshi la polisi wilayani Igunga, kupitia wapelelezi WP Paulina na WP Juliana, lilifanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo akiwa na pikipiki hiyo na wapelelezi hao waliwaleta mashahidi watano ili kutoa ushahidi wa wizi huo.

Mtuhumiwa namba mbili John Paulo alipopewa nafasi ya kujitetea alikiri kuuziwa pikipiki na mtuhumiwa namba moja (Benjamin Lawalawa) na kwa pamoja waliiomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kile walichodai wanategemewa na familia zao na pili ni kosa la kwanza na hawakukusudia kufanya hivyo ombi ambalo lilipingwa vikali na Mwendesha Mashtaka na kuiomba mahakama hiyo itoe

# Aweso akasirishwa mradi wa maji kutelekezwa

**Na Renatus Masuguliko,** BUKOMBE

NAIBU Waziri wa Maji, Juma Aweso, amegeuka mbogo baada ya kubaini mradi wa maji uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 190 wa Kijiji cha Msasa wilayani Bukombe na kukamillika mwaka 2013 umetelekezwa kwa madai ya kuibiwa pambu ya kusukuma maji.

Kufuatia majibu aliyoyapata kupitia uongozi wa Wilaya ya Bukombe, Naibu Waziri Aweso, alisikitishwa na hatua aliyodai haiwezekani mradi wa Sh. milioni 190 uliokamilika

kuanza kutoa huduma, unakatishwa kwa miaka zaidi ya mitano kutokana na kuibiwa pampu ya kusukuma maji yenye thamani ya Sh. milioni 15, wakati fedha za uendeshaji zimekuwa zinaingia kila mwaka.

"Huwezi kuanzisha mradi mpya wakati mradi uliokamilika upo tayari, lakini hautoi huduma kwa sababu ya kukosa Sh. milioni 15, hili sikubaliani nalo ninaomba uongozi wa RUWASA

wilaya kushirikiana na GEUWASA na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, kulipatia ufumbuzi hili mara moja," alisema aweso.

Pia alisema inasikitisha wastani wa upatikanaji wa maji wilayani Bukombe ni asilimia 26.8 kiwango ambacho ni cha chini na inaratarajiwa kufikia asilimia 40, mara miradi tisa kati ya 15 ya maji iliyopo kwenye programu wilayani humo itakapokamilika na akaomba nguvu za mkoa kulitazama kwa jicho la pili. Awali, akiwa wilayani Bukombe, Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba, alimweleza na kumhakikishia Waziri Aweso kuwa ni tatizo la upatikanaji majisafi na salama ni kubwa kupindukia katika mji mdogo wa Ushirombo pamoja na maeneo mengine vijijini.

"Kwa hili ninaomba msaada wa mkoa na wizara kuingilia kati mimi nimekuja hapa na kukuta haya madudu mpaka sasa hata mkoa nimeshaujulisha uwapo wa hali hiyo, miradi mingi nimeikuta hata huyo mhadisi wa maji pia naye ameyakuta," alisisitiza Nkumba.

Kutokana na takwimu zilizotolewa na kwa Waziri Aweso, inaonekana kuwa Wilaya ya Bukombe, ni kati ya wilaya nne alizozitembelea Waziri Aweso za Chato,Geita, Mbogwe na Bukombe, ndiyo yenye kiwango cha chini cha upatikanaji huduma ya maji safi na salama cha asilimia 26.8.

Hata hivyo, Waziri Aweso katika ziara yake wilayani Bukombe alipotembelea mradi wa maji wa Uyovu, alikiri kuvutiwa na kuridhishwa na uendeshwaji wake wenye akiba ya zaidi ya Sh. milioni 100 benki zinazotokana na malipo ya uchangiaji maji kutoka kwa watumiaji chini ya mwenyekiti wa kamati ya mradi huo,




Meneja Masoko na Mahusiano ya jamii wa Benki ya Exim, Bw Abdulrahman Nkondo, akichangia damu wakati wa tukio la kijamii linalofahamika kama Tanzania On Twitter lililofanyia mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Anaemuhudumia ni Ofisa Mwandamizi kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), Bw Peter Chami. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali wapewa angalizo soko la dunia

**Na Mary Geofrey**

WAJASIRIAMALI nchini wametakiwa kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha huduma zao ziendane na soko la dunia, kwa kushiriki makongamano na kubadilishana mawazo na wafanyabiashara waliofanikiwa.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwakilishi wa Kituo cha Ujasiriamali na Maendeleo ya Utendaji (CEED), Fred Laiser, katika hafla ya wafanyabiashara 40 kutoka wa ndani na nje ya nchi, waliokutana kwa lengo la kujadiliana namna ya kuboresha biashara ili kukidhi soko la dunia na namna ya kukabiliana na changamoto zilizopo. Pia, hafla hiyo iliwakutanisha wafanyabiashara mbalimbali wa mazao ya kilimo na usindikizaji vyakula walipewa mafunzo ya usimamizi, maarifa ya biashara, utayari wa uwekezaji na fursa za mtandao ili kuanzisha viwanda na kufikia lengo la kukuza uchumi wa taifa.

Laiser alisema, lengo la hafla hiyo pia ni kutoa elimu kuhusu usimamizi wa biashara zao na kuwakutanisha wajasiriamali kutoka ndani na nje ya nchi ili kujifunza namna wanavyoweza kufikia malengo yao.

"Sisi CEED kazi yetu ni kuwainua wajasiriamali mbalimbali nchini hasa wa mazao ya kilimo pamoja na mifugo. Leo tupo hapa kwa ajili ya kuwapa elimu ya usimamizi wa biashara zao hasa zinapokuwa kubwa kwasababu biashara inapokuwa kubwa changamoto nazo zinaongezeka," Fred alisema.

Kwa upande wa washiriki, Elizabeth Swai, alisema anafanyabiashara ya kuku na kwamba mafunzo hayo kutoka kwa wataalam wa kimataifa yatamuwezesha kuendeleza biashara yake.

"Kuwa mjasiriamali kuna changamoto mbalimbali, hasa kipindi ambacho biashara yako inakua changamoto zinakuwa ngumu zaidi. Kama mjasiriamali ni muhimu sana kujibadilisha mawazo kila wakati ili kutoa huduma bora au bidhaa bora kushindana katika soko". Elizabeth alisema.

Jumla ya wajasiriamali 70 nchini, wameshapata mafunzo ya usimamizi wa biashara, ushauri kitaalamu, elimu ya fedha, masoko tangu kuanzishwa kwa mpango huo mwaka 2017.



Aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Chadema wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Ambrose Ndege ambaye aliondoka na kujiunga CCM (kulia), akiwa na Diwani wa Kata ya Endiamtu, Philemon Oyogo (katikati), baada ya kurejea tena Chadema jana. PICHA: GIFT THADEY

# Wafanyakazi Tanzanite One waondolewa hofu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewatoa hofu wafanyakazi wa migodi 10 ya Kampuni ya Tanzanite One, wanaodai mishahara miezi 22 kwa kuwahakikishia baada ya kufunguliwa kwa migodi yao watapata maslahi bora.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, katika eneo la migodi hiyo, iliyopo Mirerani wilayani Simanjiro, alisema ni vema kila mmoja wao akafahamu kuwa Serikali ndio ilifunga migodi hiyo, baada ya kuona kuna hitaji la kuboresha mikataba iliyopo.

"Nikweli kufungwa kwa migodi yenu kumesababisha hali ngumu kwenu, ila nawapongeza kwa uvumilivu mlioonyesha, lakini nataka mfahamu kuwa ili dhahabu ing'ae ni lazima ipite kwenye moto na moto ndio huo mnaopitia sasa, ila endeleeni kuvumilia mtapata neema baada ya kumalizika kwa utengenezaji mikataba mingine,"alisema.

Alisema serikali ilifunga migodi hiyo ili kujipanga upya na kuangalia rasilimali hiyo itakavyoneemesha nchi kwa kupata mapato yenye tija kwa kutoza tozo sahihi badala ya kutoza asilimia nne.

Pia inataka kuhakikisha serikali inapata gawio la asilimia 16, ambayo itainua uchumi wa nchi na hatimaye kutekeleza miradi ya maendeleo.

Vile vile, alisema baada ya kumalizika kwa taratibu za kuboresha za kisheria, serikali itahakikisha wafanyakazi hao wanalipwa stahiki zao na kurudishwa kazini kama vile Rais John Magufuli anavyosisitiza utoaji ajira nchini kipaumbele ni kwa wazawa.

Nyongo pia aliagiza Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Kampuni ya TML, kuhakikisha wanalipa wafanyakazi hao ndani ya miezi mitatu, baada ya kumaliza taratibu za kumtafuta mwekezaji mwingine ambaye amepatikana na yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha.

"Pamoja waajiri wenu wameomba miezi miwili, lakini mimi nawaongezea mwezi mmoja iwe mitatu muwe mmelipwa mishahara yenu na hapo naamini kila kitu kitakuwa kimekamilika, naomba muendelee kuwa wavumilivu mlikotoka mbali na mnakoenda karibu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliwatuliza wafanyakazi na kuwataka kuondoa wasiwasi kwa sababu serikali inawalinda kila mmoja wao na kuhakikisha kila mmoja anapata haki zake stahiki.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi STAMICO tawi la Tanzanite One, Peter Salanjo, alisema kilio chao kikubwa wafanyakazi hao ni mishahara ya miezi 22 tangu Januari mwaka 2018 hadi sasa, jambo linalowafanya kuishi kwa mateso na kushindwa kumudu gharama za shule za watoto wao.

Mmoja wa wafanyakazi hao ambaye pia ni mmoja wa viongozi wa wafanyakazi katika kampuni hiyo, Antony Maswi, alimpongeza Rais kwa kuboresha miundombinu ya masuala mbalimbali na kumuomba pia kupitia maboresho inayofanya katika mgodi huo kuhakikisha wafanyakazi hao wanalipwa mishahara yao ili waondokane na mateso.

Nao wamiliki wa kampuni hiyo ambao ni wazawa wa Kampuni ya Madini ya Tanzania Limited Tanzanite One (TML), Hussein Gonga na Faisali Juma, waliwahakikishia wafanyakazi hao kuwalipa mishahara yao baada ya miezi miwili ijayo, baada ya kukamilisha taratibu za kisheria za kumpa mwekezaji mwingine ambaye kimsingi amekubali kubeba gharama zote.

Walisema pia mbali na kuwalipa katika mazungumzo wameongea naye amekubali kuwaajiri wafanyakzi hao wote katika kampuni hiyo baada ya kuanza kazi.

# Ole Nasha akisifia chuo cha Mtakatifu Joseph

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willium Ole Nasha, amekipongeza Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mtakatifu Joseph kwa kutenga zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kutoa ufadhili kwa wanafunzi 505 kwa mwaka huu wa masomo.

Vile vile, amesema fedha hizo zitasaidia kuongeza wigo wa kudahili wanafunzi wa Chuo Kikuu na kusaidia serikali katika harakati za kufadhili wanafunzi.

Akizungumza jana jijini Arusha, wakati akifunga maonyesho ya siku tatu ya teknolojia yaliyoandaliwa na chuo hicho, Ole Nasha alisema chuo hicho kinajitahidi kuendana na malengo ya serikali ya kufundisha wanafunzi kubuni miradi itakayofanikisha uanzishwaji wa viwanda.

Alisema kitendo cha chuo hicho kuhakikisha kila mwanafunzi anayesoma chuoni hapo hamalizi bila kubuni mradi utakaoleta tija kwenye jamii, ni jambo zuri na litaharakisha maendeleo ya nchi, kwa kuwa vijana hao wataenda kujiajiri na kuwa waajiri. Alitoa wito kwa vyuo vingine nchini kuiga mfano huo kwa kuhakikisha wanafunzi wanabuni vitu vitakavyoleta tija katika jamii hata baada ya wao kumaliza masomo yao.

"Pamoja fedha hizi zitanufaisha wanafunzi wanaojiunga na chuo hiki tu, lakini kama serikali tunapongeza sababu wataongeza idadi ya wanachuo wanaojiunga na vyuo vikuu," alisema. Pia, aliwaasa wanafunzi wanaoomba maombi ya kujiunga na vyuo vikuu nchini kuhakikisha wanajaza fomu zao wenyewe badala ya kuwaachia watu walioko kwenye Internet ambao baadhi yao hawana uelewa wa kujaza fomu hizo na kusababisha wakose mikopo au vyuo kwa kukosea.

"Mkijaza wenyewe mtakuwa makini, lakini mkiachia watu wa migahawa au Internet watajaza kimakosa sababu hawana maslahi na hicho kitu unachoomba," alisema.

Aliiagiza Tume ya Sayansi na Teknolojia kuangalia ubunifu unaofanywa katika chuo hicho na kusaidia kupeleka katika utekelezaji wa miradi kwa kuwasaidia wanafunzi hao.

"Hapa nimeona ubunifu mwingi wa miradi zaidi ya 250 sasa hii ikipata ufadhili na kuboreshwa tutasaidia wanafunzi wetu kupata miradi na jamii kupata ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili na ipo miradi mingi mipya Tume ya Sayansi na teknolojia njoni muone vitu vipya msaidie kuanzisha miradi ya uzalishaji," alisema.

Rais wa Chuo hicho, Dk. Thomson Ananth, alisema fedha zilizotengwa kwa ajili ya ufadhili wa wanafunzi hao zitasaidia 505 kati ya hao 300 wa kike. Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Innocent Ngalinda, alisema wameamua kutoa ufadhili huo kusaidia wanafunzi ambao wanatoka familia duni zisizo na uwezo wa kulipia mikopo.

Pia alisema wanatoa kipaumbele kwa wanafunzi bora kitaifa wa kidato cha nne na sita watakaojiunga na chuo chao kwa kulipiwa ada.

"Lakini ufadhili huu hatutaki mtoto abweteke kila mwaka wa pili atawekwa kwenye mchujo kwa kuangalia kiwango cha ufaulu wako, hivyo lazima ujitahidi kusoma ili uendelee na ufadhili wetu kwa miaka mitano," alisema.

## Arumeru yapunguza vifo vya mama na mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI wilayani Arumeru imefanikiwa kupunguza vifo vya mama na mtoto, baada ya kuboresha huduma za afya wilayani humo, ikiwamo dawa na vifaa muhimu vinavyotumika wakati mama anajifungua.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum ya kitaifa ya kuzuia vifo vya mama na mtoto, inayojulikana kwa jina la ' Jiongeze, tuwavushe Salama', iliyofanyika katika ofisi za Halmashauri ya Meru, Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo wilayani Arumeru, Dk. Maneno Focus, alisema huduma hizo zimeboreshwa kwa asilimia 98.

"Katika wilaya yetu tunataka kutokomeza vifo vya mama na mtoto na tunafanya hivi kwa vitendo, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2019, tumepata vifo viwili pekee vya watoto ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018, watoto watano walikuwa wamefariki," alisema. Hata hivyo, alisema pamoja na takwimu hizo bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati, kutoka kwenye jamii hususani kwa wazazi ambao hawafiki kwenye vituo vya afya kwaajili ya kupata huduma.

Dk. Maneno alisema kampeni hiyo imelenga kuongeza uwajibikaji wa viongozi wa kisiasa, kidini, kijamii na wadau wote kuwajibika na kuhakikisha vifo vya mama na mtoto vinadhibitiwa na kufuatiliwa na kila mmoja kushiriki kuvizuia.

"Halmashauri ya Meru inatarajia kuongeza huduma jumuishi za kujifungulia (Ce-Monc), katika kituo cha afya cha USA – RIVER, ambacho majengo ya huduma muhimu yamekamilika, tunaamini hadi kufikia mwakani hakutakuwa na vifo vya mama wala mtoto wilayani kwetu,"alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro alisema, Wilaya ya Arumeru, imeazimia kuboresha huduma za afya na mikakati iliyopo ni kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha afya na kila kijiji kinakuwa na zahanati.

Muro aliwaagiza viongozi wa Hospitali ya Meru, kuweka katika mbao za hospitali matangazo ya katazo la watendaji wa afya hospitalini hapo, kutumia simu wakati wa kazi na kuwataka kutumia lugha nyenyekevu kwa wagonjwa na kwa kufanya hivyo, utekelezaji wa kaulimbiu ya kampeni hiyo ya 'jiongeze tuwavushe salama' itakuwa imetekelezwa vizuri.





# Waziri aagiza kiwanda kurekebisha mishahara

**Na Mary Mosha,** SAME

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ameagiza ifikapo Agosti 15, mwaka huu, viwango vya mishahara katika kiwanda cha kuchakata mkonge cha Hassan Sisal Estates kilichoko Same, viwe vimerekebishwa.

Kiwanda hicho kinamilikiwa na Kampuni ya Mohamed Enterprises (MeTL) na kina wafanyakazi 500 katika mashamba ya mkonge.

Akizungumza jana baada ya kukutana na menejimenti na wafanyakazi wa kiwanda hicho, Waziri Mhagama alizitaka mamlaka husika kuhakikisha kabla ya tarehe hiyo wawe wamemaliza kazi ya kutoa elimu juu ya viwango vya mishahara, upimwaji wa afya na kuundwa kwa vyama vya wafanyakazi.

"Mbali na kupewa elimu na kuanzisha vyama vya wafanyakazi, hakikisheni wafanyakazi wote wanapimwa afya zao, kabla na baada ya kumaliza kazi na watendaji wote wapewe vifaa vya usalama kazini. NSSF (Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii) natoa wiki mbili mhakikishe mmepokea malipo yote kutoka kwa waajiri wao," aliagiza.

Julai 19, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alimwagiza Waziri Mhagama kwenda katika kiwanda hicho kushughulikia haraka malalamiko ya wafanyakazi hao ambao wanadai kunyonywa mishahara yao kampuni za uwakala za Upami na Unique.

Pia alimtaka waziri huyo kupitia upya mikataba ya ajira ya wafanyakazi hao na kujiridhisha kama inalingana na kazi wanayoifanya na ikiwezekana asimamie ifumuliwe na kuandikwa upya.

Aidha, Mshauri na Meneja wa Kiwanda hicho, Ndekirwa Nyarialiahidi, aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo hayo yaliyotolewa na Waziri Mhagama kabla ya tarehe husika.

Akiwa katika kiwanda hicho, Meneja wa Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) wa Kanda ya Kaskazini, Juma Maneno, alimhakikishia waziri kuwa atazipatia ufumbuzi changamoto zilizowasilishwa kwake, kabla ya tarehe husika.

# DC apiga 'stop' uuzaji ndizi changa

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

SERIKALI imezuia uvunaji na uuzaji wa ndizi changa katika Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro na kuagiza maofisa ugani na Halmashauri ya Wilaya hiyo kuanza udhibiti wake hasa katika soko la Mamsera.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, alieleza masikitiko yake jana moja mfupi kabla hajazindua machapisho mbalimbali yanayohusu mradi wa uboreshaji wa migomba wilayani humo, unaotekelezwa kwa miaka minne na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari-Tengeru).

"Tunasema ndizi ni chakula, ajira na biashara lakini nimetembelea kwenye masoko nimekuta ndizi changa zinavunwa, labda mniambie ni sawa sawa kuvuna ndizi changa? Inatakiwa pale kwenye migomba ikae muda gani? Naambiwa na wataalam pale inapozaa inategemea, lakini ni miezi mitatu. "Ukienda pale Kariakoo shimoni (Dar es Salaam), utakuta milima ya ndizi na maparachichi yanayotoka Rombo na yanayotoka katika maeneo mengine, lakini tunaambiwa kwa kiasi kikubwa yanatoka kwetu na hasa yanayouzwa soko la Mamsera," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Hokororo ameagiza maofisa ughani na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, kuanza kudhibiti uvunaji huo, akisema anadhani ni muhimu kufanya hivyo kwa sasa ili kuwa na uhakika wa chakula.

"Najua wakulima na wananchi huwa hawapendi tukidhibiti, lakini naomba niwashawishi tunapovuna mazao machanga tunapata hasara kwa sababu huwezi kwenda kuiuza katika ile bei ambayo umeitarajia. Lakini pia tunajitengenezea njaa, suala la kuwa na uhakika wa chakula kama ambavyo wataalam wanasema linaweza kuwa changamoto, uache kuvuna ndizi changa," alisisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), Dk. Geofrey Mkamilo, Meneja wa Tari-Tengeru, Dk. Stephano Kuoko, alisema mradi wa kuboresha migomba katika Wilaya ya Rombo ulianza kutekelezwa mwaka 2017 na utafikia ukomo mwaka 2020. Kwa mujibu wa Dk. Kuoko, mradi huo wa unafadhiliwa na Taasisi ya Kimataifa ya Bill & Melinda Gates na washirika ambao ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Kawanda-Uganda (NARO) na Tari.

Katika mradi huo unaowahusisha pia wadau wengine ambao ni Taasisi ya Kimataifa ya Mazao ya Kitropiki (ITTA), Biodiversity na Cabi ambayo inajishughulisha na usambazaji wa taarifa na kufikisha teknolojia kwa wakulima, kata zilizoguswa na mradi huo ni Mamsera, Chala, Mengwe, Mengeni, Mandan na Aleni.

"Matarajio yetu ni watu kubadilika kiuchumi, kwamba watabadilika sasa kwa sababu watakuwa wakizalisha ndizi kwa kutumia mbinu bora zaidi na za kisasa zaidi. Uzalishaji wa ndizi utaongezeka, kama ulivyoona kwamba sasa hivi wastani ni kama tani 10 kwa kila hekta moja ya ndizi, lakini sisi tunalenga ikibidi hata kufikisha tani 69," alisema Dk. Kuoko



Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, akizungumza na wananchi wa kata ya Kirumba Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza mwishoni mwa wiki wakati alipomwakilisha mkuu wa mkoa huo, John Mongella, katika kufunga kampeni ya 'nyumba ni choo' iliyoanza Julai 7 na kufika katika kata 30 na kuhitimishwa Julai 26, kampeni hiyo inaendelea kupita kila mkoa ambapo siku ya jumapili 28 itaanza Mkoa wa Mara. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Pombe yaelezwa chanzo homa ya ini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

DAKTARI Bingwa wa magonjwa ya ndani na mbobezi wa uchunguzi wa homa ya ini wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Dk. Elichilia Shao, amesema matumizi ya pombe kali ni moja ya sababu zinazochangia kwa kiasi kikubwa mtu kupata maambukizi ya ugonjwa wa homa ya ini.

Akizungumza jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini katika viwanja wa hospitali hiyo, Dk. Shao alisema ugonjwa huo unasababishwa na vitu mbalimbali ikiwamo virusi vya Hepatitis B na C na maambukizi mengine ya bakteria kama fangasi (kuvu) na matumizi ya pombe kali.

"Homa ya ini ni tofauti na ule ugonjwa wa manjano, tunachanganya. Watu wanafikiri mara nyingi kwamba maambukizi ya Hepatitis B au C ambayo inaleta shida kwenye macho yanakuwa na manjano, kwamba ile homa ya manjano ndiyo homa ya ini.

"Si kila mtu mwenye manjano kwenye mapafu yake kwamba ana maambukizi ya virusi vya Hepatitis B au C. kuna vyanzo vingine vingi vinaweza kusababisha manjano kwenye macho ikiwemo saratani ya kongosho na magonjwa mengine ya virusi, ni tofauti. Kitu kingine kinaweza kuleta madhara ni dawa ambazo mtu anatumia kwani anaweza kupata manjano kwenye macho yake," alisema.

Duniani kote watu milioni 257 wanaoishi na virusi vya Hepatitis B kulinganisha na watu milioni 37 wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Kwa Tanzania ukubwa wa maambukizi ni asilimia 4.5 licha ya kwamba imejitahidi kutoa chanjo.

Kihistoria, Hepatitis B iligundulika mwaka 1967 na chanjo yake iligundulika mwaka 1969. Tangu hapo chanjo yake imekuwa ikifanya kazi tangu miaka ya 80 na kwa miongo mitatu sasa, kuna chanjo ambayo inaaminika na ambayo inatusaidia kuepuka watu wasipate maambukizi ya homa ya ini.

Kwa mjibu wa Mkuu wa Idara ya Uhusiano ya KCMC, Gabriel Chisseo, kwa siku moja tu ya Julai 27 ambayo Hospitali ya Rufaa ya KCMC na Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMCo) kilipoendesha upimaji, wananchi waliojitokeza walifikia 1,100 na kwa siku ya pili walitarajia kupokea zaidi ya wananchi 2,000.

Katika maadhimisho hayo, Katibu Mtendaji wa Shirika la Msamaria Mwema (GSF) na Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya KCMC, Dk. Gilleard Masenga, alitangaza 'neema' kwa wazee 20 watakaogundulika hawana maambukizi ya homa ya ini kuwa watapewa chanjo bure.

Dk. Massenga alisema kwa Tanzania ukihesabu watu 100, wanne kati yake wana tatizo la homa ya ini. Alisema Hospitali ya Rufaa ya KCMC, Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro na Taasisi ya Utafiti ya KCMC kwa pamoja wameona umuhimu huo na wameamua kugharamia vipimo na utoaji wa elimu kwa jamii ya Watanzania katika kuunga mkono serikali ya Rais Dk. John Magufuli.

NIPASHE JUMATATU JULAI 29, 2019

Nipashe
Spotika



## ZILIZOPANDA NA KUREJEA ZITAHIMILI VISHINDO VYA LIGI? UK.18



# NAKUACHA...

Kiungo wa Manchester United, Paul Pogba (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Inter Milan, Samuele Longo, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa wiki iliyopita. United ilipata ushindi wa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**


## ISIKUPITE

Mwekezaji wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mohammed Dewji 'MO' amesema hana nia yoyote ya kuondoka katika klabu hiyo na kuwataka wanachama na mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi kutokuwa na wasiwasi. Mfanyabiashara huyo pia amewataka mashabiki wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi katika Tamasha la Simba Day litakalofanyika Agosti 6 mwaka huu.



# MASTAA

## WANAOSAKA UHAMISHO KWA UDI NA UVUMBA




**LONDON, England**

NAHODHA wa Arsenal, Laurent Koscielny aligoma kusafiri na timu kwenye kwenye ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani.

Dirisha la usajili wa majira ya joto barani Ulaya linaendelea kupamba moto na tayari kuna usajili wa mamilioni ya pauni unaohusisha wachezaji wenye majina makubwa umefanyika.

Tayari miamba ya soka Hispania klabu ya Barcelona imemsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann kutoka klabu pinzani ya Atletico Madrid kwa kitita cha euro milioni 120.

Atletico kwa upande wao wametumia kitita cha pauni milioni 126 kumsajili Joao Felix mwenye miaka 19 kutoka Benfica ya Ureno.

Lakini kama ilivyokuwa katika misimu iliyopita, kuna nyota wakubwa ambao wanataka kuhama ama wanahusishwa na uhamisho wa fedha nyingi lakini mpaka sasa bado hakuna kilichofikiwa.

Kuna nyota ambao wanaonekana kusaka uhamisho kwa nguvu zote. Nyota hao wamegoma kuungana ama wameachwa na timu zao katika kipindi hiki cha kujiandaa na msimu mpya wa 2019/2020.

Laurent Koscielny

Huyu ni nahodha wa washika bunduki wa London klabu ya Arsenal.

Koscienly mwenye miaka 33 alijiunga na Arsenal mwaka 2010 na bado yungali na mkataba na klabu hiyo mpaka mwishoni mwa msimu wa 2019/2020.

Hata hivyo, ameweka wazi nia yake ya kutaka kuondoka klabuni hapo katika dirisha hili la usajili.

Nahodha huyo ameenda mbali kwa kufikia hatua ya kugoma kusafiri na timu kwenye kwenye ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani. Katika taarifa kwa vyombo vya habari, Arsenal ilieleza kusikitishwa kwake na hatua hiyo ikisema ni "kinyume kabisa na maelekezo yetu kwa mchezaji."

Klabu tatu za nchini Ufaransa Bordeaux, Rennes na Lyon zimeonesha nia ya kutaka kumsajili mchezji huyo.

Inaarifiwa kuwa Bordeaux imempa ofa ya mkataba wa miaka mitatu.

Mchezaji nyota wa zamani wa Arsenal, Ian Wright amemtahadharisha Koscienly kuwa matendo yake ya sasa yatamfanya afute kumbukumbu zote nzuri alizojijengea kwenye mioyo ya mashabiki wa Arsenal kwa miaka 9.

**Mauro Icardi**

Tofauti na Koscienly, Icardi alivuliwa unahodha wa klabu yake Februari mwaka huu.

Icardi naye hayupo kwenye kambi ya maandalizi ya Inter Milan na mshambuliaji huyo anatarajiwa kuuzwa kwenda klabu nyengine hivi karibuni.

Icardi amekubaliana na uongozi wa klabu hiyo kutokuwa sehemu ya kambi ya maandalizi.

Juventus ndiyo imekuwa ikitajwa zaidi katika mbio za kumsajili lakini mpaka saasa hakuna mazungumzo rasmi yaliyofanyika.

Napoli pia wanahusishwa na kumtaka sawia na AS Roma japo itakuwa vigumu kwa Icardi kwenda Roma ambao hawatashiriki Klabu Bingwa Ulaya msimu ujao.

**Pogba na Lukaku**

Alipoulizwa na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki iliyopita juu ya mustakabali wake katika kikosi cha Man United, Lukaku akajibu: "subirini wiki ijayo mtajua kitu."

Lukaku amekuwa akihusishwa na kuhamia katika klabu ya Inter Milan na imefahamika kuwa uhamisho wake utategemea na kitakachotokea kwa Icardi.

Hivyo endapo Icardi atauzwa wiki hii ni dhahiri kuwa uhamisho wa Lukaku kujiunga na klabu hiyo utakuwa umeiva.

Lukaku ameambatana na kikosi cha United kwa sasa kilichopo kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya nchini Australia na Singapore.

Mshambuliaji huyo hakuwa na wakati mzuri msimu uliopita na amekuwa akishutumiwa kwa kushuka kiwango.

Kwa upande wa Pogba kumekuwa na sarakasi za kutosha na zilikolea pala mchezaji huyo aliposema mwezi uliopita kuwa "sasa inaweza kuwa muda mzuri wa kuhamia sehemu nyingine".

Ni dhahiri kuwa si kocha Ole Gunnar Solskjaer wala uongozi wa Man United unaotaka mchezaji huyo nyota kuondoka Old Trafford katika dirisha hili la usajili la majira ya joto.

Wiki iliyopita, wakala wa mchezaji huyo Raiola aliliambia gazeti la The times kuwa mchezaji wake anataka kuondoka, na klabu hiyo inajua fika nia ya mteja wake.

Vilabu vya Real Madrid na Juventus vinaripotiwa kutaka kumsajili kiungo huyo Mfaransa mwenye miaka 26 japo hakuna kati yao ambaye amepeleka maombi rasmi ya kutaka kumnunua.

**JE, WAJUA?**

TIMU ya Azam FC ya jijini Dar es Salaam ambayo ilianzishwa mwaka 2008, imefanikiwa kucheza fainali za Kombe la Kagame mara tatu mfululizo na ikichukua taji hilo mara mbili mfululizo.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA

## Ozil na Kolasinac wavamiwa na majambazi

WACHEZAJI wa Arsenal, Mesut Ozil na Sead Kolasinac wameripotiwa kuvamiwa na genge la majambazi katika jaribio la wizi wa gari katika barabara za mji wa London nchini England.

Klabu ya Arsenal imethibitisha kuwa wachezaji wake Ozil na Kolasinac walilengwa na majambazi hao waliokua wamejihami, lakini hawakujeruhiwa katika tukio hilo.

Kanda ya video iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii inamuonesha Kolasinac akipigana na na wanaume wawili waliokuwa wamejihami kwa visu.

Mchezaji huyo pia anaonekana akiruka kutoka kutoka kwenye gari kukabiliana na wanaume waliokuwa wameficha nyuso zao na ambao walikuwa na njama ya kuwaibia.

Msemaji wa polisi wa jiji la London amesema: "Tumepata taarifa kuwa washukiwa waliokuwa juu ya pikipiki walijaribu kumuibua mtu aliyekuwa akiendesha gari.

Hakuna mshukiwa yeyote aliyekamatwa kufikia sasa .

Kolasinac na Ozil ni wachezaji wa kwanza wa soka kuvamiwa katika barabara za London.





Bwalya


Kagere

# SIMBA NA YANGA ZIMESHINDWA KUWASAJILI HAWA

Na Adam Fungamwango

TAYARI klabu za Simba na Yanga zimepeleka majina ya wachezaji watakaowatumia kwa msimu ujao wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Kombe la Shirikisho.

Zimebaki pia siku chache tu kabla usajili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukamilike. Usajili wa Ligi Kuu utakamilika Julai 31 mwaka huu.

Lakini kwa hali jinsi ilivyo ni kwamba Simba na Yanga hazitoongeza mchezaji yoyote kwenye Ligi Kuu badala yake zitawatumia wale wale ambao majina yao yamepelekwa CAF kwenye ligi pia.

Wanachama na mashabiki wa klabu hizo wameshajua majina ya wachezaji wote, wa kigeni na wa kibongo.

Hata hivyo kuna baadhi ya majina ambayo awali yalikuwa yanatajwa kutaka kusajiliwa na klabu hizi kwa nyakati tofauti, lakini hazikufanikiwa kwa sababu moja au nyingine.

Moja ya sababu ni kushindwa dau, kuwa na mikataba na klabu zao, kuwahiwa na klabu zingine na sababu zingine zinazofanana na hizo.

Hawa ndiyo baadhi ya wachezaji ambao saini zao zilikuwa zinahitajiwa sana kwa klabu za Simba na Yanga, lakini zikaota mbawa.

**1. Walter Bwalya-Simba**

Ni msimu wa tatu sasa wanachama na mashabiki wa Simba wanaimba jina la mchezaji huyu. Ni straika hatari wa Nkana FC na msimu uliopita aliichezea timu hiyo dhidi ya Simba na kufunga bao pamoja na timu yake kutolewa.

Msimu huu ilionekana Simba kuwa karibu zaidi kumsajili kiasi hata baadhi ya magazeti kuandika kuwa tayari dili limekamilika.

Hata, hivyo taarifa kutoka ndani ya Simba zikasema kuwa klabu hiyo imeshindwa kutokana na dau kubwa lililotajiwa kutoka kwa klabu ya Nkana FC.

Taarifa zilizotoka kabla ya kwenda mitamboni ni kwamba tayari Bwalya, raia za Zambia mchanganyiko na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), amemwaga wino kwenye klabu ya El-Gouna ya nchini Misri.

**2. Meddie Kagere-Yanga**

Kocha Mkuu wa Yanga Mwinyi Zahera alisema kabla hajaondoka aliacha maagizo kwa viongozi kama kuna uwezekano kumsajili straika hatari wa Simba, Meddie Kagere kwa ajili ya msimu ujao wa ligi.

Hata hivyo, maagizo hayo yalikuwa magumu mno kama vile ngamia kupenya kwenye tundu la sindano, kwani ndiyo kwanza alikuwa anamaliza mkataba wa mwaka mmoja na Simba kati ya miwili aliyosaini. Na kama vile haitoshi, ameongezewa mingine miwili, hivyo kwa sasa ana mkataba wa miaka mitatu na kuivunja kwa klabu hiyo ni ngumu.

**3. Justin Shonga-Simba**

Siku ya mwisho ya usajili wa (Caf) kulitokea tetesi za Simba kuwa katika hatua za mwisho kumsajili straika matata Justin Shonga, raia ya Zambia ili kuziba nafasi ya Emmanuel Okwi.

Hata hivyo, tetesi za usajili wa mchezaji huyo zilianza kuyeyuka kama moshi wa sigara hewani na mpaka sasa Simba imebaki na wa idadi ile ya wachezaji 27 tu, huku straika huyo akiripotiwa kubaki wa timu yake ya zamani ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

**4. Jonas Mkude-Yanga**

Kiungo huyu wa Simba ambaye kwa sasa yuko na kikosi cha timu ya taifa, Taifa Stars, naye alitakiwa kwenye orodha ya wachezaji wanaotakiwa na Zahera.

Akasema ili timu itishe msimu ujao, inatakiwa imsajili Mkude. Hata hivyo imemkosa kwani tayari ameongeza mkataba wa miaka miwili na Simba baada ya ule ya kwanza kumalizika.

**5. Godfrey Walusimbi-Simba**

Akiwa kwenye fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon)nchini Misri, Godfrey Walusimbi alionyesha kiwango cha juu na zikatoka taarifa za kutakiwa na klabu ya Simba kutaka kumsajili. Walusimbi ambaye anacheza beki wa kushoto, ilisemekana kuwa anasajiliwa ili kusaidiana na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' kwani imeachana na Asante Kwasi.

Hata hivyo, usajili wa Gadiel Michael umezima ndoto hizo za kumsajili beki huyo ambaye baada ya mkataba wake na Kaizer Chiefs kumalizika mwaka huu.

**6. Salum Aiyee-Yanga**

Ni straika ambaye ameshika nafasi ya pili kwa ufungaji bora msimu uliopita akiwa na magoli 19, nyuma ya Mnyarwanda Kagere aliyemaliza na magoli 23.

Aiyee aliyekuwa akiichezea Mwadui FC, alitajwa kuwa angesajiliwa na Yanga kuwa mbadala ya Mkongomani Heritier Makambo ambaye amesajiliwa na klabu ya Horoya FC.

Wakati kila mmoja akitarajia kumuona akitia saini kwenye klabu ya Yanga, akaibukia kwenye klabu ya KMC na kuzima ndoto za Yanga kuipata saini yake.

**7. Ramadhani Kapera-Simba**

Baada ya kuwahenyesha kwenye mechi zote mbili za msimu uliopita ambazo Simba ilifungwa, benchi la ufundi na viongozi wa Simba walivutiwa mno na winga Ramadhani Kapera.

Hata hivyo, kwa mastaajabu ya wengi, aliibukia kwenye klabu ya KMC na kutia kandarasi, na ndoto za Simba kumpata zikayeyuka.

**8. Khassim Hamisi-Yanga**

Mpaka sasa haijajulikana kama amesajiliwa na KMC au Azam FC, lakini klabu zote mbili zilikuwa zinahitaji saini yake. Hata hivyo kabla ya KMC na Azam FC kumkomalia Yanga ilikuwa ikimhitaji kwa udi na uvumba. Lakini ilionekana kama upepo umebadilika, baada ya kuanza kusajili zaidi wachezaji kutoka nje ya nchi kuliko wazawa.

**9. Haruna Shamte-Simba**

Wakati dirisha la usajili likifunguliwa kulikuwa na taarifa ya Simba kutaka kumsajili beki wake wa zamani Haruna Shamte. Ni baada ya kuonyesha kiwango kizuri, akiwa na Lipuli FC.

Ilitajwa kuwa Simba ilimtaka beki huyo kwa ajili ya kusaidiana na Shomari Kapombe ambaye ni majeruhi wa mara kwa mara. Hata hivyo, dili hilo limebuma.

**10. Lucian William 'Gallas'**

Kulikuwa na taarifa za Yanga kumtaka kiungo huyo ili kuimarisha eneo la kati, lakini kadri siku zilivyozidi kusonga mbele ndiyo taarifa hizo zilivyokuwa zinafifia.

Mwishoni akaibukia kwenye klabu iliyopanda daraja msimu huu Polisi Tanzania, akitokea Lipuli FC yeye na kocha wake Suleiman Matola.

# NYOTA 11 WA KUCHUNGWA LIGI KUU ENGLAND 2019/20




**LONDON, England**

HUKU msimu mpya ukitarajiwa kuanza mwezi ujao, kuna wachezaji wengi vijana ambao wameonyesha vipaji vyao kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya.

Kila timu ina wachezaji ambao inatarajia msimu huu watang'ara zaidi na pengine kuwa nyota wakubwa.

Makala hii inakuchambulia wachezaji 11 vijana ambao wanatarajiwa kung'ara zaidi msimu huu wa Ligi Kuu 2019/20.

Joao Virginia

Anajulikana kama mtafsiri lugha kwa wachezaji wanzake pale Everton ambao hawajui kiingereza, akiwasaidia kama Bernard, Richarlison na wachezaji wengine, lakini Joao Virginia ambaye ni golikipa anatajwa kwamba ana nafasi kubwa ya kung'ara msimu huu.

Kabla ya kujiunga na Everton, Virginia alitumia muda wake kucheza katika timu za vijana za Benfica na Arsenal.

Kocha, Marco Silva ameonekana kuwa na imani kubwa na kipa huyo mwenye umri wa miaka 19 na msimu huu unaweza kumtoa zaidi.

Reece James

Huyu ni kinda wa Chelsea ambaye msimu uliopita alikuwa akicheza kwa mkopo kule Wigan Athletic, ambako aliibuka mchezaji bora wa msimu katika klabu hiyo.

Ingawa yeye ni beki wa kulia, lakini James amekuwa akifurahi zaidi kucheza katika nafasi ya kiungo wa kati.

**Aarons**

Wakati Norwich ikipanda ligi msimu uliopita alikuwa akicheza kama beki wa kulia, ingawa anaweza pia kucheza nafasi nyingine.

Alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na Manchester United, lakini baada ya kusajiliwa kwa Aaron Wan-Bissaka ataendelea kuichezea timu yake hiyo msimu huu.

Taylor Harwood-Bellis

Msimu huu atakuwa akikipiga pale Manchester City na anaonekana kujulikana na mashabiki wengi wa timu hiyo.

Katika umri wake wa miaka 17, tayari beki huyo ameonekana kuwa na kiwango cha kuvutia katika mechi za maandalizi ya msimu huu na ana nafasi kubwa nyota yake kung'ara msimu huu.

**Eric Garcia**

Huyu ni mhitimu kutoka akademi ya soka ya Barcelona iitwayo La Masia, na ni wazi kuwa msimu huu ana nafasi kubwa zaidi ya nyota yake kupaa kwenye Ligi Kuu England akiwa na Manchester City.

Kocha Pep Guardiola tayari ameonyesha imani kubwa kwa Mwanakatalunya mwenzake huyo, na alimwanzisha kwenye mechi zote mbili za nusu fainali ya kombe la Carabao dhidi ya Burton Albion msimu uliopita.

**Oliver Skipp**

Mashabiki wa Tottenham Hotspurs wana matumaini makubwa kwa Oliver Skipp ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 18, kwani kwa muda mfupi aliopewa nafasi ya kucheza ameonyesha kiwango cha kuvutia.

Kocha Mauricio Pochettino kwa sasa anakuwa na nafasi nzuri ya uchaguzi wa viungo katika kikosi chake hasa baada ya ujio wa Tanguy Ndombele, lakini Skipp anaonekana kuwa kwenye mipango ya kocha huyo.

**Morgan Gibbs**

Huyu ni kiungo wa timu ya Wolverhampton Wanderers ambaye anaonekana kuwa makini mno dimbani na alikuwa na wakati wa kuvutia msimu wa 2018/19.

Amekuwa anacheza nyuma ya washambuliaji kwa kusaidia kupeleka mbele mashambulizi. Alifunga bao wakati wakiibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Newcastle kwenye mechi za mandalizi ya msimu mpya.

**Phil Foden**

Nyota Phil Foden ameonekana kumvutia Guardiola kwa kiwango chake pale Manchester City na ana nafasi kubwa ya kuwa kwenye kikosi cha kwanza msimu huu.

Guardiola mara kwa mara amekuwa akimtaja Foden kama ni almasi ya England, kwani kiwango chake kimekuwa kikimkosha mno.

Amekuwa akicheza nyuma ya mabeki hasa unapotumika mfumo wa 4-3-3.

**Reiss Nelson**

Kwenda kucheza kwa mkopo katika Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, akiwa na timu ya Hoffenheim pengine ndio kitu bora zaidi alichokifanya Reiss na sasa msimu huu atakuwa katika jezi za Arsenal.

Alicheza jumla ya mechi 29 msimu wa 2018/19, na pia alipata uzoefu wa kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha Unai Emery ana nafasi nzuri ya kumtumia Nelson msimu huu katika safu ya ushambuliaji.

**Callum Hudson-Odoi**

Huyu ni mchezaji wa timu ya taifa ya England ambaye anatajwa kuwa na mafanikio makubwa siku za usoni.

Hudson-Odoi amekubali kuongeza mkataba wake pale Chelsea na sasa msimu huu ana nafasi nzuri zaidi ya kuwika.

Msimu uliopita hakupewa nafasi ya kucheza kwenye mechi nyingi na kulikuwa na uvumi kwamba anakwenda Bayern Munich.

Lakini sasa chini ya kocha mpya, Frank Lampard baada ya kuondoka kwa Maurizio Sarri aliyejiunga na Juventus anaweza kupata nafasi nyingi zaidi ya kucheza.

Kocha Lampard tayari amemhakikishia nafasi katika kikosi chake msimu huu hali iliyomfanya akubali kusaini mkataba mpya wa miaka mitano.

**Mason Greenwood**

Huyu ni kinda mshambuliaji wa Manchester United na tayari ameonekana kumkuna vilivyo kocha wake Solskjaer na msimu huu ana nafasi kubwa mno ya kuwa kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Katika mechi za maandalizi ya msimu mpya ameonekana kuwa gumzo kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia katika mechi dhidi ya Leeds United na Inter Milan.

Mashabiki wengi wa Manchester United sasa wanamtaka dogo huyo awe katika kiko-

## Nukuu


"Tunamtaka na tungependa Leroy Sane abakie na kuna ofa inayosubiri ya kuongeza mkataba wake, ila bado uamuzi wa kubaki au kuondoka hapa uko chini yake, iwapo anataka kuondoka anaweza kufanya hivyo lakini hatutafurahia," **alisema Kocha wa Manchester City, Pep Guradiola akiwaambia waandishi wa habari juu ya winga huyo Mjerumani.**



"Napenda ushindani, hakika naupenda. Nadhani ni jambo zuri kwa klabu kuwapo kwa ushindani. Kukiwa na wachezaji wazuri katika nafasi yako unalazimika kufanya kazi kwa juhudi zaidi kila siku, hasa mazoezini, hilo linaisaidia timu kwenda kwenye levo za juu zaidi," **alisema Victor Lindelof kuhusu kuwania namba katika kikosi cha Manchester United.**



'Nilipata ofa nyingi lakini niliamua kujiunga na Fenerbahce kwa sababu ninaamini nitakuwa na furaha zaidi nikiwa pale. Nimezungumza na wachezaji mbalimbali wa timu hiyo na wao wamenisaidia kufanya uamuzi," **mshambuliaji Mjerumani Max Kruse wenye umri wa miaka 31 ambaye alikuwa anawindwa na Liverpool alisema.**



## Michezo



Kikosi cha Kagera Sugar ambacho kiliponea chupuchupu kushuka daraja msimu huu na kurejea Ligi Kuu kwa mfumo wa 'play off'.

# ZILIZOPANDA NA KUREJEA ZITAHIMILI VISHINDO VYA LIGI?

**Na Adam Fungamwango**

REKODI za Ligi Kuu Tanzania kwa miaka ya hivi karibuni zinaonyesha kuwa kati ya timu tatu au nne zinazopanda daraja, moja lazima ishuke kwa msimu huo huo.

Mfano mdogo ni African Lyon ambayo ilipanda na kuanza kucheza Ligi Kuu Bara msimu wa 2018/19 na msimu huo huo ikateremka daraja.

Kama rekodi hii itaendelea na msimu ujao, basi tutarajie moja kati ya timu za Namungo FC au Polisi Tanzania ikishuka daraja.

Na kama siyo hizo, basi zile timu zilizokwenda kucheza mechi maalum za 'play off', Kagera Sugar au Mwadui moja wapo itaaga Ligi Kuu.

Kati ya timu hizi nne ni timu gani itarekemka daraja mwishoni mwa msimu wa Ligi Kuu 2019/20?

Hata hivyo, rekodi siku zote zipo ili zivunjwe, inawezekana kwa mara ya kwanza baada ya misimu zaidi ya mitatu mpaka minne tunashuhudia hakuna timu yoyote iliyopanda daraja msimu huu ikashuka.

Pamoja na hayo, ili rekodi zisijirudie, inabidi timu hizi kufanya kazi ya zaida, ikiwamo kusajili wachezaji wazuri.

Nikisema wazuri nina maana wenye uwezo mkubwa kisoka, si mradi tu mchezaji aliyekuwamo kwenye kikosi kilichoipandisha timu kucheza Ligi Kuu.

Zinatakiwa pia ziwe na wachezaji wazoefu kwenye Ligi Kuu, benchi la ufundi lenye ujuzi, pamoja na klabu kuwa na uwezo wa kifedha.

Wakati mwingine timu inaweza kuwa na kila kitu, lakini ikakosa uwezo wa kifedha, hivyo wachezaji wanakosa posho na mishahara, hivyo kushusha morali na kuanza kufanya vibaya.

Mwandishi wa makala haya anaziangalia timu hizi ambazo rekodi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinawaweka kwenye wakati mgumu.

**1. Namungo FC**

Hii ndiyo timu pekee ambayo wengi hawaipi nafasi ya kushuka msimu ujao, na badala yake mashabiki wengi wanaipa nafasi kubwa ya kufanya vema na kutingisha kwenye Ligi Kuu.

Ni kwa sababu ilivyojipanga ndani na nje ya uwanja. Maandalizi yake tu kucheza Ligi Daraja la Kwanza ilizishinda hata baadhi ya timu zinazocheza Ligi Kuu.

Haikushangaza kuona kuwa ndiyo timu ya kwanza kabisa kupanda Ligi Kuu msimu huu na itacheza kwa mara ya kwanza.

Timu hii ina maskani yake mkoani Lindi na itatumia Uwanja wa Kassim Majaliwa.

Hata hivyo, haitakiwi kujiamini sana kwa sababu mara nyingi Ligi Kuu huwa ni ngumu zaidi kuliko Ligi Daraja la Kwanza kwa sababu huku juu, Namungo itakuwa ikicheza dhidi ya timu kongwe zenye kila aina ya staili za kutafuta ushindi kama Simba, Yanga na Azam, lakini pia timu zenye uzoefu kama Mtibwa Sugar na zingine, hivyo inabidi ikaze msuli ili isalie.

**2. Polisi Tanzania**

Ni timu nyingine iliyopanda msimu huu. Imeonyesha kama vile nayo imejidhatiti kuja kuleta ushindani na upinzani kwenye Ligi Kuu. Imemchukua mmoja wa makocha mashuhuri nchini, Suleiman Matola kutoka Lipuli na baadhi ya wachezaji kwenye uwezo mkubwa kutoka huko.

Ni mara ya kwanza kwa timu hii kupanda kama ilivyo Namungo, lakini pia inawakilisha timu zote za Jeshi la Polisi Tanzania nchini.

Ina kazi ya kufanya kwenye Ligi Kuu kwani, mbali na ile rekodi mbaya ya timu zinazopanda ni lazima moja iteremke, lakini pia timu za majeshi mbalimbali kama vile Prisons inayomilikiwa na Magereza, JKT Tanzania inayomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa kwa miaka ya hivi karibuni zimekuwa hazina ushindani na si imara kama zilivyokuwa miaka ya nyuma.

Kwa maana hiyo, Polisi Tanzania itabidi ijidhatiti, vinginevyo inaweza kurejea ilipotoka kama haikukaa vizuri.

**3. Kagera Sugar**

Achana na habari za kushushwa daraja kimakosa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), timu hiyo ilibidi irejee Ligi Kuu Tanzania baada ya kwenda kucheza 'play off' na timu ya Pamba ya Mwanza.

Baada ya kutoka sare ugenini, ilishinda nyumbani mabao 2-1 na kurejea kwenye Ligi Kuu.

Tatizo kubwa la timu hiyo ni kwamba inaonekana kukamia baadhi ya mechi, hasa na Simba na kuwa timu ya kawaida inapocheza na timu zingine.

Hali hii ndiyo iliyosababisha iponee chupuchupu. Kwa sasa ipo kwenye Ligi Kuu. Imerudi katika zile nafasi nne za timu kupanda. Hivyo rekodi ya timu zinazopanda na kushuka bado haiiepuki kama ikifanya masihara.


**4. Mwadui FC**

Kama ilivyo Kagera Sugar, Mwadui nayo imeponea chupuchupu na ingekwenda moja kwa moja Daraja la Kwanza kama isingeshinda kwenye mechi ya 'play off', dhidi ya Geita FC.

Ni moja ya timu ambayo ilifanya vizuri kwenye mzunguko wa kwanza, lakini iliondokewa na baadhi ya wachezaji wake kwenye kipindi cha dirisha dogo na kuanza kudorora.

Msimu unaokuja inabidi ijifunge mkanda kisawasawa kwani ipo kwenye zile nafasi mpya nne za kupanda Ligi Kuu, ila tu yenyewe si timu mpya ila imechukua nafasi ya zile timu zilizowekewa kupanda. Ina maana rekodi hii ya timu tatu au nne ya timu zinazopanda moja huwa inashuka, nayo inamhusu.

**NAJUA WAJUA**



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco, ameteuliwa kuwa nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inashiriki mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

SOKA

# MAKINDA 6 WANAOSTAHILI NAMBA UNITED



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ina utamaduni tajiri wa kuibua na kupaisha vipaji vya wachezaji vijana, wakiwa wanamkuza mchezaji mzawa kwenye kila msimu kuanzia Oktoba mwaka 1937.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer anaujua vizuri utamaduni huo, tangu akianza kucheza chini ya Sir Alex Ferguson.

United tayari ina wachezaji vijana wengi ambao wanaweza kuwapandisha katika kikosi cha kwanza na hapa tunawaangalia wachezaji sita ambao wanastahili kuwa kwenye kikosi cha kwanza msimu huu 2019/20.

**Lee O'Connor**

Beki huyu mzaliwa wa pale Waterford, Lee O'Connor amekuwa na kikosi cha United tangu mwaka 2016 na amekuwa akifananishwa na John O'Shea, kwa staili yake ya uchezaji.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 18, msimu uliopita aliingizwa kwenye kikosi cha United chini ya umri wa miaka 23 na amekuwa akiimarika vizuri zaidi kwa uchezaji. Ana nafasi kubwa msimu huu unaokuja kuingia kwenye kikosi cha kwanza cha United.

**Dylan Levitt**

Ingawa aliachwa kwenye kikosi cha United kilichokwenda kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya nchini Australia, Dylan Levitt, mwenye umri wa miaka 18 alikuwa akifanya mazoezi na kikosi cha kwanza kabla hakijapaa.

Nyota huyo wa kimataifa wa Wales anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi cha kwanza cha Solskjaer na msimu unaokuja anastahili kuwa kwenye kikosi cha kwanza. Ameitwa kwenye kikosi cha Wales na kocha Ryan Giggs.

**James Garner**

Chipukizi, James Garner mwenye umri wa miaka 18 amekuwa akifananishwa na kiungo wa zamani wa United, Michael Carrick baada ya kuanza kuichezea timu ya wakubwa msimu uliopita wakati akiwa na umri wa miaka 17. Na akapewa mkataba mpya ambao utamweka hapo hadi mwaka 2022 ikiwa ni siku chache kabla hajatimiza umri wa miaka 18.

Kutakuwa na ushindani mkubwa kwenye safu ya kiungo msimu huu, lakini Garner tayari ameshajiimarisha na kuuthibitisha uwezo wake dimbani. Na pia ameonyesha kiwango kizuri kipindi hiki cha ziara ya maandalizi ya msimu mpya kwa kufunga bao kwenye mchezo dhidi ya Perth Glory.

**Tahith Chong**

Tahith Chong ni mchezaji bora wa mwaka kijana kwa msimu wa 2017/18 na msimu uliopita alicheza mechi nne kwenye kikosi cha kwanza na amekuwa na kiwango cha kuvutia kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 19 anaonekana kujiimarisha vizuri na kuna uwezekano mkubwa kwa kocha Solskjaer kumweka kwenye kikosi cha kwanza msimu huu.

**Angel Gomes**

Hivi karibuni atasherekea kutimiza miaka 19 na Angel Gomes alianza vizuri kwenye kikosi cha vijana cha United na msimu huu ana nafasi kubwa ya kuingia katika kikosi cha kwanza.

Hakuna shaka kwamba, msimu huu atakuwa na nafasi nzuri ya kuthibitisha ubora wake, kwani hata klabu kama Barcelona ilikuwa ikimwania msimu huu kumsajili na ameonyesha kiwango cha kuvutia kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya.

Mason Greenwood


Bado ana miezi mitatu ili afikishe umri wa miaka 18, lakini tayari Solskjaer amethibitisha kwamba Mason Greenwood ana nafasi ya kuanza kwenye mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea.

Kinda huyo ambaye alicheza mechi nne katika kikosi cha kwanza msimu uliopita, ameonekana kuimarika zaidi hasa kwenye mechi za hivi karibuni za kujindaa na Ligi Kuu England.

"Ana nafasi ya kuanza kwenye mechi dhidi ya Chelsea kwa uhakika kabisa. Ana uwezo mkubwa. Kwani anajua kutafuta mabao akiwa eneo la hatari, hivyo ana nafasi ya kuanza," alisema Solskjaer wakati akimzungumzia kinda huyo kwenye ziara nchini Australia.

Greenwood pia amekuwa akisifiwa na wachezaji wenzake kama Marcus Rashford, ambaye aliingia kwenye kikosi cha kwanza mwaka 2016 na sasa amekuwa chaguo la kwanza kwa kocha Solskjaer katika kikosi hicho."

NDANI YA 18



THAMANI ya beki wa Spurs, Toby Alderweireld, ambaye anawaniwa na Manchester United sasa itaongezeka kutoka dau la awali la pauni milioni 25. Hayo ni makubaliano yaliyowekwa kwenye mkataba wake.



HUKU msimu mpya ukitarajiwa kuanza mwezi ujao, kuna wachezaji wengi vijana ambao wameonyesha vipaji vyao kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya.

Uk. 16-17

# AFCON 'IMEKULA' MAKOCHA HAWA



Amunike

**CAIRO, Misri**

HERVE Renard ameamua kujiuzulu kama kocha mkuu wa Morocco baada ya timu hiyo kutolewa mapema katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019).

Morocco ni mojawapo wa timu zilizopigiwa upatu kabla ya kuanza kwa mashindano hayo huko nchini Misri, lakini ilishindwa kupitia mikwaju ya penalti na Benin katika hatua ya timu 16 bora.

Renard, raia wa Ufaransa, amewahi kushinda mataji mawili ya Afcon akiwa na Zambia (2012) na Ivory Coast mnamo 2015, alikiongoza kikosi cha Morocco tangu Februari mwaka 2016.

"Umewadia wasaa wa mimi kuufunga ukurasa huu mrefu na mzuri katika maisha yangu," amesema Renard mwenye miaka 50 mara baada ya kujiuzulu.

Katika taarifa kwenye mtandao wa kijamii, Renard amesema, "Ni uamuzi usioweza kuepukika ulichukuliwa hata kabla ya kuanza mashindano ya Afcon 2019.

"Nilichukua uamuzi huu bila shaka baada ya kutafakari kwa makini. kwa hivyo siwezi kuugeuza."

Renard aliitoa Morocco kutoka nafasi ya 81 katika orodha ya Fifa duniani hadi katika nafasi ya 47.

Hata hivyo, Renard siyo kocha wa kwanza kuondoka au kuondolewa kutokana na matokeo duni katika mashindano hayo yaliokamilika mwaka huu.

**EMMANUEL AMUNIKE**

Mapema Julai mwaka huu, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilitangaza kusitisha mkataba na kocha, Emmanuel Amunike.

Taarifa fupi iliyotolewa na TFF ilidai kuwa Amunike amekubaliana na TFF kusitisha mkataba huo.

Amunike alipewa kibarua cha kuinoa Tanzania maarufu kama Taifa Stars Aprili mwaka jana.

Atabakia kwenye historia ya mpira Tanzania kwa kuiongoza nchi hiyo kufuzu fainali za Afcon, ikiwa ni baada ya kuzikosa fainali hizo kwa miaka 39.

Kabla ya hapo alinyanyua Kombe la Dunia mwaka 2015 akiwa kocha wa timu ya vijana wa chini ya miaka 17 ya Nigeria.

Kocha huyo ni winga wa zamani wa timu ya taifa ya Nigeria na klabu ya Barcelona.

Hata hivyo, Amunike alikuwa akilaumiwa na baadhi ya mashabiki kwa namna anavyoteua wachezaji na kupanga kikosi.

Tanzania ilitolewa katika mashindano ya Afcon baada ya kupoteza michezo yote ya makundi, ikicheza dhidi ya mabingwa Algeria, Senegal na majirani zao Kenya.

**SEBASTIEN DESABRE**

Mfaransa Sebastien Desabre aliachia nafasi ya ukocha wa Uganda kwa ridhaa yake baada ya timu yake kuiaga michuano ya Afcon.

Uganda ilipoteza kwa kufungwa bao 1-0 na Senegal jijini Cairo katika mchezo wa hatua ya 16 bora.

Shirikisho la Soka Uganda (Fufa), lilisema Desabre ameondoka huku akiwa amebakiwa na miezi mitano kumaliza mkataba wake.

"Fufa inatoa shukrani kwa mchango wa Desabre kwenye maendeleo ya soka la Uganda na timu ya Uganda Cranes," ilisema taarifa hiyo.

Desabre mwenye umri wa miaka 42 amekuwa kocha wa Uganda tangu aliposaini mkataba wa miaka miwili kuinoa timu hiyo mwezi Desemba mwaka 2017.

Kabla ya Cranes kupoteza mbele ya Senegal, wachezaji waligomea mazoezi, mzozo uliokuwa kati ya wachezaji na Fufa kuhusu malipo.

JAVIER AGUIRRE

Misri imemng'oa Javier Aguirre baada ya wenyeji kufungwa katika hatua ya 16 bora katika mashindano hayo ya Afcon.

Mafarao hao kama wanavyojiita, walipigiwa upatu pia kabla ya kuanza kwa mashindano hayo lakini ilifungwa bao 1-0 mjini Cairo baada ya bao alilosukuma Thembinkosi Lorch wa Afrika kusini kunako dakika ya 85.

Rais wa Shirikisho la Soka Misri, Hany Abo Rida pia alijiuzulu akisema lilikuwa ni 'jukumu la kimaadili'.

Aguirre, ambaye ni raia wa Mexico mwenye umri wa miaka 60, alijiunga na kikosi hicho cha Misri mwaka jana akichukua mikoba ya Hector Cuper, aliyeondoka baada ya kushindwa katika fainali za Kombe la Dunia.

**CLARENCE SEEDORF**

Aliyekuwa mchezaji wa kiungo cha kati wa Uholanzi, Clarence Seedorf, alitimuliwa kama kocha wa Cameroon baada ya upande wake kushindwa kulitetea taji la Afcon mwaka huu.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid mwenye umri wa miaka 43, alikuwa mkufunzi kwa chini ya mwaka mmoja.

Seedorf alisema angefurahia kuendelea na alihisi kuwa kikosi chake kimeonyesha matumaini.

Alisaini mkataba wa miaka minne kukiongoza kikosi cha Simba wasiofugika mnamo Agosti mwaka 2018.

Lakini taarifa ilithibitisha kwamba "shirikisho la soka Cameroon kwa mujibu wa vifungu katika mikataba yao imeamua kusitisha mkataba wa Seedorf na msaidizi wake Patrick Kluivert".

**USILOLIJUA**



Nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos amesema bado wanaendelea kumtambua Gareth Bale ni mchezaji wa timu hiyo na wanafuraha kuendelea kuwa naye kwenye kikosi hicho, kila mchezaji ana uamuzi kuhusu hatima yake.



# Kurusha watoto kunasababisha kifafa, matatizo ya akili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KINAMAMA wameshauriwa kuacha tabia ya kuwarusha au kuwatikisa watoto wadogo chini ya miaka miwili kwa sababu ni hatari, kunasababisha madhara makubwa ikiwamo ugonjwa wa kifafa na magonjwa ya akili.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi, Dk. Khamis Ally, wakati wa mahojiano na waandishi wa habari wanawake wa Mkoa wa Mbeya, waliotembelea hospitali hiyo kwa lengo la kuwasalimia kinamama na watoto waliolazwa hospitalini hapo.

Dk. Ally alisema, baadhi ya kinamama wamekuwa na utaratibu wa kuwatikisa au kuwarusha watoto wao pindi wanapojifungua au nyakati nyingine kwa lengo la kuwachangamsha, alisema sio jambo jema kwa kuwa lina madhara kwa mtoto kwa sababu ubongo wake na utosi haujakomaa hivyo unasababisha mtikisiko wa ubongo na kusababisha kizunguzungu na baadaye kupata ugonjwa wa kifafa au akili yake kutokuwa sawa hapo baadaye.

"Hizi tabia za kutikisa au kuwarusha watoto wanaozaliwa au walio na umri chini ya miaka miwili sio utaratibu mzuri, jamii inapaswa kuacha kwa sababu ubongo wa mtoto na utosi wake haujakomaa anapaswa kufanyiwa hivyo kuanzia miezi 18 nawasihi kuachana na imani potofu kuwa kuwarusha watoto inaondoa degedege badala yake inaleta degedege na matatizo mengine ya akili," alisema Dk. Ally.

Aliongeza kuwa mbali na jamii kuacha tabia ya kuwarusha watoto, lakini wajawazito wanapaswa kujifungulia kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali ili kuepusha madhara kwa mtoto.

Alisema miongoni mwa madhara yanayoweza kuepukika kwa kujifungulia kwenye huduma za afya ni mtoto kuzaliwa salama bila tatizo lolote la ubongo.

Alisema kinamama wengi wanaojifungulia nyumbani hawapati huduma stahiki na kuna uwezekano wakati wa kujifungua mtoto akiminywa kichwa na hivyo kusababisha madhara hapo baadaye.

Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi, Stella Mhina, aliwashauri wananchi hususani vijana kuacha tabia ya unywaji wa pombe kupita kiasi kwa kuwa ni miongoni mwa sababu za ugonjwa wa kifafa.

Alisema baadhi ya wagonjwa wanaotibiwa kifafa hospitalini hapo, ugonjwa umesababishwa na ulevi kutokana na ubongo huvurugika na kusababisha kifafa.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasole, alipongeza mafanikio yaliyopatikana katika hospitali hiyo ikiwamo ukarabati wa majengo kwenye wadi mbalimbali za wagonjwa. Alisema chama kinatambua mchango wao na kitaendelea kutoa ushirikiano na kuwasihi kuendelea kuwahudumia wagonjwa kwa moyo wa upendo.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbolea ya YARA Tanzania, Winstone Odhiambo (Kushoto), akimkabidhi hati ya makubaliano mmoja wa wasambazaji wa mbolea ya YARA kutoka Makambako Agrochemical, Bernadetha Sanga, katika mkutano uliofanyika jijini Dar es salaam mwishoni mwa wiki uliowakutanisha mawakala na wasambazaji wote wa mbolea ya YARA nchini kwa lengo la kufanya tathmini na kupeana malengo ya msimu wa kilimo wa mwaka 2019/20. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafurahia vyama vya ushirika zao la kokoa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

BARAZA la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya limepongeza hatua ya Serikali ya kuanzisha vyama ushirika kwenye zao la kokoa na kupitia vyama hivyo, wakulima wamenufaika.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Dk. Hunter Mwakifuna, wakati wa Kikao cha Baraza la Madiwani na kusema sasa wakulima wanafurahia matunda ya kilimo cha zao la kokoa baada ya serikali kuwaunganisha pamoja kupitia vyama vya Ushirika.

Dk. Mwakifuna alisema vyama vya msingi vimesaidia kupunguza wimbi la wanaonunua Kokoa za wakulima kwa bei ya chini wakati wao wanaingiza faida kubwa na kwamba baada ya vyama vya ushirika sasa kilo moja huuzwa Sh. 4,200 badala ya Sh. 3,000.

"Hakika sasa tunajivunia kuanzishwa kwa vyama vya ushirika katika zao la kokoa mimi ni miongoni mwa wanufaika kwa sababu nauza kokoa zangu kwenye ushirika kwa bei ya kuridhisha," alisema Dk. Mwakifuna.

Aliwasisitiza wakulima kutokukubali kushawishika kuuza kokoa kwa njia ya panya maarufu 'Njemke' badala yake wauze kwenye soko la pamoja la ushirika ambalo husaidia kuuza kwa bei itakayowanufaisha.

Pia, aliwataka wataalam wa kilimo katika Wilaya ya Kyela kuwatembelea wakulima wa kokoa na kuwapa elimu ya namna ya kuhudumia zao hilo ambalo linahitaji uangalizi wa hali ya juu.

Alisema wakulima wengine hulima kilimo cha mazoea hivyo wataalam wanajukumu la kuwaelekeza wakulima njia bora ya kulima na kuvuna kokoa ili ziwe katika ubora ambao unaendana na mahitaji ya soko.

Diwani wa Kata ya Ikimba, Katule Kingamkono, alisema madiwani wataendelea na umoja wa kupinga utoroshwaji na uuzaji holela wa zao hilo ili kuhakikisha mkulima anauza mazao yake kwa bei elekezi.

# Mbarali waahidiwa machinjio ya kisasa

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, imeahidi kujenga machinjio ya nyama katika Kata ya Lugelele ili kuwaondolea adha watumiaji na wauzaji wa kitoweo hicho kusafiri kufuata huduma hiyo katika maeneo mengine.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi wa wilaya hiyo, Emmanuel Kishimbo, Ofisa Mipango, wakati akijibu swali la Mwenyekiti wa Kijiji chaIgomelo kilichopo Kata ya Lugelele, Frank Motombaya, kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Igomelo, Frank Motombaya, aliwauliza viongozi wa halmshauri ni lini watapeleka huduma ya machinjio kwenye Kata yao ili kuondokana na adha ya kutumia gharama kufuata huduma hiyo maeneo mengine licha ya kuwa tayari wametenga eneo kwa ajili ya kutolea huduma hiyo.

Motombaya alilieleza Baraza kuwa kwa sasa wauzaji wa nyama hufuata kitoweo hicho kwenye machinjio ya Rujewa na kuuza katika bucha zao na kwamba nyama hiyo haikai muda mrefu kutokana na uhitaji na uwapo wa machinjio utasaidia huduma hiyo kupatikana kwa uhakika.

Kaimu Mkurugenzi, Kishimbo alisema wilaya inafahamu hitaji hilo na kwamba baada ya bajeti ya mwaka huu kupangwa na fedha kupatikana, watafungua machinjio katika eneo hilo.

"Nimepokea maombi hayo na naahidi kufikisha kwa wahusika muhimu ni kwamba ofisi ya mkurugenzi inafahamu uhitaji huo na tutajitahidi kulishughulikia fedha zitakapopatikana," alisema Kishimbo.

Naye Ofisa Mifugo, Eusebius Mbidah, alisema eneo la ujenzi wa machinjio limetengwa wanachosubiria sasa ni kupagwa kwa bajeti ili wakutane na kujadili namna ya ujenzi huo.

Aliwaomba wananchi wa kata ya Lugelele kuwa wavumilivu wakati michakato mingine ikiendelea na kwamba waendelee kutumia machinjio ya Rujewa.



# RPC aomba msaada vitendea kazi

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, ameziomba taasisi na wadau kulisaidia Jeshi la Polisi vitendea kazi mbalimbali ili kuliwezesha kupambana na uhalifu .

Muroto alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki ofisini kwake alipokuwa akipokea msaada wa pikipiki mpya mbili zilizotolewa na kiwanda cha kutengeneza pikipiki cha Wuzhou Investment Limited cha Mkurunga mkoani Pwani.

Alisema jeshi hilo linafanya kazi saa 24 na vitendea kazi vilivyopo havitoshelezi kufika kila mahali, hivyo misaada inahitajika ili kuifikia jamii maeneo mengi. “Serikali peke yake haiwezi kumaliza changamoto za mahitaji ya jeshi letu kutokana na gharama kubwa za kuhudumia jamii, hivyo wadau na jamii inahitajika kusaidia,”alisema.

Pia aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo kwa kuwapelekea taarifa na kuwafichua wahalifu walioko kwenye maoneo yao ili hatimaye wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Naye Mkurungenzi Msaidizi wa Wuzhou Investment Ltd, Raymond Huang, alisema kutokana na umuhimu wa jeshi hilo, wameona wasaidie vitendea kazi ili kupambana na uhalifu.

Huang alisema kiwanda hicho kilianzishwa mwaka 2015 na kimekuwa kikisaidia jeshi hilo vitendea kazi hivyo kutokana na kujua faida ya amani iliyopo.

Aliongeza kuwa tangu mwaka jana hadi sasa kampuni hiyo imetoa pikipiki 25 katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo hilo la kuzidi kuimarisha ulinzi.

Alitaja maeneo hayo na idadi ya pikipiki kwenye mabano kuwa ni Njombe (10), Morogoro (moja), Dar es Salaam (nane), Dodoma (mbili), Pwani (nne).

Pamoja na msaada huo, Huang alisema kiwanda hicho kitaendelea kulisaidia jeshi hilo vifaa na vitendea kazi ili kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia unaendelea kuimarishwa.



Mkulima wa zao la zabibu, Maria Pesambili mkazi wa Kijiji cha Hombolo Nje kidogo ya Jiji la Dodoma mkoani Dodoma, akikagua zao aina ya zabibu nyeupe kama alivyokutwa kijijini hapo jana, wakulima hao wamelalamikia kukosa uhakika wa soko la zao hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakiwa kutenga maeneo bidhaa za ngozi

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (Sido) limeziomba mamlaka za serikali za mitaa kutenga maeneo ya wafanyabiashara wa bidhaa za ngozi ili kupata masoko kwa urahisi.

Meneja msimamizi wa mradi wa kituo cha mafunzo ya ngozi kutoka Sido Dodoma, Stephano Ndunguru, alitoa rai hiyo jana wakati akifunga mafunzo kwa wajasiriamali yaliyofanyika kwa wiki sita jijini hapa.

Ndunguru alisema bidhaa za ngozi ni muhimu na zina thamani kubwa, hivyo wajasiriamali wa aina hiyo wanahitaji kuwa na eneo lao ili kuzitangaza bidhaa zao kwa jamii inayowazunguka.

“Serikali ya mtaa inapaswa kushirikiana na Sido ili kusaidia kutengeneza ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya ujasiriamali kupitia vikundi wanavyounda ambavyo tayari wanakuwa wamepata utaalamu,” alisema.

Alisema lengo lao ni kuona washiriki wa mafunzo wanapata faida ya ujuzi waliopewa na wataalam wa utengenezaji wa viatu, mikanda ya kuvaa, mikanda ya mbwa na bidhaa zingine nyingi ambazo hutumia ngozi.

Ndunguru alisema Sido imekuwa mstari wa mbele kutoa mafunzo kwa wajasiriamali lakini changamoto kubwa inayowakabili wajasiriamali ni kukosa maeneo ya kuziweka biashara zao ili kuonekana kirahisi na jamii inayohitaji.

“Tunaomba serikali za mitaa zitenge maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara wa bidhaa za ngozi kwa sababu zina thamani kubwa na zinahitaji kutangazwa”, alisema Ndunguru.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Burhan Magandila, alisema mafunzo hayo yatawezesha kuwa na viwanda vidogo vya bidhaa za ngozi huku akiiomba serikali kuwekeza kwenye eneo hilo.

Magandila alisema Sido imetoa mchango mkubwa kwa vikundi vya wajasiriamali ambavyo hivi sasa wengine wanashiriki katika maonyesho ya biashara ya ndani na nchi na nje.

Alitoa wito kwa vijana wenzake ambao wanabweteka mitaani bila kazi yoyote wajitokeze kushiriki mafunzo ya ujasiriamali na hatimaye kujiajiri.

Naye Hagai Wille kutoka Kongwa, alisema awali ilikuwa vigumu kwake kutengeneza bidhaa za ngozi lakini baada ya mafunzo hayo, amejipanga kushiriki maonyesho ya biashara kupitia bidhaa anazotengeneza.

# Watangaza kuweka mgombea urais 2020

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Wakulima (AAFP), Rashid Rai, amesema chama chake kitaweka wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu, pamoja na wa urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Rai aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa ofisi ya makao makuu ya chama hicho jijini hapa alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema chama hicho kimejipanga kuhakikisha kuwa kinashiriki kwa kuweka wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

“Sisi katika uchaguzi wa serikali za mitaa tumejipanga kikamilifu kushiriki katika nafasi zote zinazogombewa lakini pia katika uchaguzi mkuu tutaweka mgombea katika nafasi ya urais” alisema Rai.

Aidha, Raia aliwataka wananchi kuhakikisha wanajitokeza kujiandikisha katika uboreshaji wa daftari la wapigakura ambalo linaendelea sasa.

“Niwaombe Watanzania kote nchini uboreshaji huu unapofika katika maeneo yao wahakikishe wanajitokeza katika kujiandikisha ili kupata haki yao ya kupiga kura na kumchagua kiongozi wanayemtaka,” alisema.

Pia aliishauri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kuongeza nguvu katika kutoa elimu kwa wananchi ili wawe na uelewa juu ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Rai alisema mpaka sasa umebaki muda mfupi lakini hajaona jitihada za Tamiseni kutoa elimu ya zoezi hili la uchaguzi wa serikali za mitaa hali ambayo inaweza kuchangia watu wengi kutoshiriki.

Katibu huyo pia aliipongeza serikali ya awamu ya tano kwa jitihada zake za kuboresha miundoimbuni mbalimbali ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa na vituo vya afya.

Naye Mkurugenzi wa Watu wenye Ulemavu wa chama hicho, Donge Said Donge, aliwataka Watanzania katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu kuwapa nafasi ya kuongoza watu wenye ulemavu.

Alisema watu wenye ulemavu nchini, bado wanakumbana na changamoto kubwa hasa katika suala elimu kutokana na shule ambazo zanaweza kuwahudumia watu wenye mahitaji maalumu kuwa hazitoshi.





# Waziri ataka wananchi kuuenzi utamaduni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wananchi kutambua kuwa rasilimali kubwa katika maisha ya mwanadamu ni pamoja na utamaduni.

Akizungumza wakati wa kilele cha ufungaji wa tamasha la 24 la utamaduni wa Mzanzibari, katika Uwanja wa Gombani, Chakechake Pemba, alisema utamaduni pia ni kielelezo na utambulisho wa maisha ya kijamii.

Alisema asiyethamini utamaduni wake ni sawa na mtumwa wa utu na akili yake, asipokubaliana na mfumo wake wa maisha kuna hatari ya kufanya mambo yasiyokubalika katika jamii yake.

Alisema ni vyema mfumo waliolelewa wazazi wa kuwa na heshima, utu, adabu, ustaarabu na maadili mema kuwarithisha na watoto wao kwa kuwa ndio utakaowasaidia kuujua utamaduni wao na kuwa na mwenendo nzuri wa maisha yao.

Alieleza kuwa kaulimbiu ya mwaka Huu ya "Utamaduni ni ngao ya ustawi wa maisha yetu" inakumbusha kuwa kila mmoja atekeleze majukumu yake katika kuulinda, kuuenzi na kuuendeleza utamaduni wa nchi, kwa kuwa majukumu hayo yanapopuuzwa husababisha mtafaruku katika jamii.

Hata hivyo, aliiomba jamii kufikiria upya matumizi bora ya fani mbalimbali za kiutamaduni na sanaa na namna zitakavyowaletea maendeleo.

Alisema utamaduni una fursa za kipekee kwa faida za kiuchumi na kijamii na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika ilani yake ya Chama cha Mapinduzi imeweka wazi kutekeleza dhamira hiyo ya kuuenzi utamaduni wa nchi.

Pia aliiomba Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutanua wigo wa ushiriki wa wanafunzi, kwa kusaidia kukuza na kuendeleza kwa pamoja vipaji vya sanaa na utamaduni kwa wanafunzi na kuweka jukwaa lao la ngoma, tamthilia, tenzi, ngonjera, mashairi, nyimbo kutoka shule mbalimbali Unguja na Pemba.

Kwa upande wake Katibu wa Shirikisho la Wasanii kisiwani Pemba, Salum Nassor Salum, alisema mafanikio mengi yameweza kupatikana kwa wasanii tokea kuanzishwa kwa Wizara ya Vijana, hivyo amempongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, pamoja na viongozi wa wizara hiyo na kuwaonba kuendelea kuwaunganisha wasanii kwa lengo la kuukuza utamaduni nchini.

# Wanawake kuwezeshwa kumiliki ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wametakiwa kupewa elimu na kuwezeshwa ili kumiliki mali kisheria.

Hayo yameelezwa na mwanasheria kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Mohammed Khamis, wakati akiwasilisha mada juu ya sera na sheria ya ardhi huko katika ofisi ya Chama cha Wanahabari Tanzania (Tamwa) ofisi ya Zanzibar, Tunguu.

Alisema asilimia kubwa ya wanawake hawajui sheria za umiliki mali hususani ardhi hali inayosababisha migogoro wanapoachana na mwenza wao.

Alisema katika tafiti mbalimbali duniani mwanamke asilimia kubwa anachangia katika shughuli za uzalishaji mali hususani katika kilimo, lakini wanashindwa kumiliki kisheria ardhi hizo wanazoendesha shughuli zao za kilimo.

Alisema Zanzibar kunasheria nyingi na nzuri, lakini jamii hawazifahamu hivyo ipo haja kwa serikali kupitia wizara husika inayoshughulikia ardhi kuendelea kuwapatia elimu jamii ili waweze kumiliki ardhi zao kihalali na kuepusha migogoro inayowakumba wanawake wengi.

Alisema miongoni mwa sheria hizo ni za uhaulishaji wa ardhi, wananchi wengi wanatakiwa kujua hasa suala la uhaulishaji wa ardhi.

Hata hivyo, alisema wanawake wengi wa Zanzibar wanategemea zaidi ardhi za kurithi kutoka kwa wazazi wao hivyo kutokuwa na hati za umiliki wa ardhi ndipo migogoro inapotokea.

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wezake waliohudhuria mafunzo hayo, Faidari Fumu, kutoka kijiji cha Matemwe alisema asilimia kubwa hawana uwelewa wa kumiliki ardhi hali iliyopelekea kuwa na ardhi pasipo kufuata sheria.

Alisema kuwa changamoto inayowafanya kutomiliki ardhi hizo kisheria ni kuwapo kwa kiwango kikubwa cha fedha katika taratibu za kumiliki ardhi kisheria hali inayosababisha baadhi yao kushindwa kumudu gharama hizo kutokana na umaskini wa kipato.

Naye meneja mtetezi na sera kutoka Tamwa, Hawra Shamte, alisema chama hicho kinatoa mafunzo mbalimbali kwa wanawake ili waweze kumiliki ardhi kisheria.



Mafundi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka jijini Dar es Salaam (Dawasa), wakifanya maandalizi ya kubadilisha bomba la maji taka katika mtaa wa Ali Hassan Mwinyi jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# SMZ kudhibiti mlipuko homa ya ini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema inaendelea na mapambano dhidi ya homa ya ini ili kudhibiti mlipuko wa ugonjwa huo kabla haujawa janga la kitaifa.

Akizungunza katika uzinduzi wa chanjo ya homa ya ini Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid, alisema kipaumbele cha mapambano hayo kimeanza kwa wajawazito, watu wa makundi maalumu na wafanyakazi wa afya Zanzibar.

Alisema makundi hayo yataaanza kupatiwa chanjo hiyo kwa sababu imethibitika kuwa makundi hayo yapo hatarini zaidi kupata maambukizi ya homa ya ini na ni rahisi zaidi kuyasambaza kwa wengine.

Vile vile Hamadi alisema hali ya ugonjwa na vifo vinavyotokana na athari za homa ya ini duniani vinaongezeka kila mwaka na serikali baada ya kuona hivyo imeungana na nchi mbalimbali duniani kwa lengo la kuondoa homa hiyo kwa kuwa ni tishio kwa afya na jamii.

Hamad aliwataka waandishi wa habari kuelimisha wananchi umuhimu wa chanjo hiyo ili kujikinga na ugonjwa wa homa ya ini inayosumbua ulimwenguni hasa bara la Afrika na zaidi kwenye nchi zilizo chini ya jangwa la Sahara ikiwamo Zanzibar.

Alisema bado Zanzibar haujafanywa utafiti wa moja kwa moja, lakini ni bora wananchi wakakubali kukingwa kabla ya ugonjwa huo haujaenea zaidi na takwimu za mwaka 2015 zinaonyesha wastani wa watu milioni 257 wanaishi na maambukizi ya ini B na milioni 71 homa ya ini C duniani.

Hamadi alisema serikali ina lengo la kuondoa ugonjwa huo na ndio maana wizara inashirikiana na sekta mbalimbali ndani na nje ya nchi, wadau na wataalamu katika kutekeleza mpango mkakati huo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Marijan Msafiri, alisema ugonjwa wa homa ya ini ni hatari hivyo ushirikiano unahitajika ili kupambana na ugonjwa huo kwa wananchi kukubali kupatiwa chanjo hiyo.

Alisema mtu anaweza kupata maambukizi ya ini na kuugua kwa muda mfupi na kupona kwa miezi sita na endapo itazidi ndani ya miezi hiyo basi atakuwa na homa ya ini sugu.

Naye Mkurugenzi Kinga na elimu ya afya Zanzibar, Dk. Fadhili Mohamed Abdalla, alisema lengo la kutolewa chanjo hiyo ni kukinga ugonjwa huo usiweze kuenea kwa wingi Zanzibar.

Alisema tayari serikali imejipanga kwa kila hatua ikiwamo vifaa vya kufanyia kazi katika mapambano hayo ya homa hiyo. Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Ghirmay Andemichael, aliiahidi serikali kuwa shirika hilo litaendelea kuiunga mkono Wizara ya Afya kuhakikisha ugonjwa huo unatibiwa na kuondoka nchini Zanzibar.

Uzinduzi huo ni miongoni mwa maadhimisho ya siku ya homa ya ini ambayo hufanyika Julai 28, kila mwaka duniani na kaulimbiu "Tuwekeze katika kuondoa homa ya ini Zanzibar.

# TBS yatoa fursa kwa wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wajasiriamali nchini kuchangamkia fursa ya kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha kwenye shirika hilo bure.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa TBS Kanda ya Kusini, Haji Mussa, wakati akitoa mada kwenye semina iliyofanyika maonyesho ya viwanda na Kongamano la uzalishaji lililofanyika katika Uwanja wa Majimaji, Mjini Songea kusuhu majukumu ya Shirika katika kuwezesha biashara, viwanda na utaratibu wa kupata alama ya ubora wa TBS.

Maonyesho hayo yaliyoanza Julai 24, mwaka huu, yalifunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa,

Julai 25, mwaka huu. "Kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, TBS kwa kushirikiana na serikali bado linaendelea kuthibitisha ubora wa bidhaa bure kwa muda wa miaka mitatu kama ilivyokuwa awali," alisema Mussa na kuongeza:

"Mjasiriamali atapata barua ya utambulisho kutoka SIDO itakayomwezesha kuthibitishiwa ubora wa bidhaa zake bure."

Alisema kufuatia uamuzi wa serikali kwa bidhaa za chakula na vipodozi kushughulikiwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) sasa utaratibu wa kupata alama ya ubora ya TBS umerahisishwa.

Kwa mujibu wa Mussa mwombaji anatakiwa kutuma maombi yake TBS na Shirika litafanya pia ukaguzi wa majengo na kwamba hiyo imepunguza changamoto walizokuwa wanakutana nazo.

Awali, bidhaa za chakula na vipodozi zilikuwa chini ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

Alisema maonyesho hayo yameandaliwa na Mkoa wa Ruvuma, lengo likiwa ni kuonyesha fursa za uwekezaji zinazopatikana mkoani Ruvuma na kuwakutanisha wazalishaji na watoa huduma wanaowezesha biashara.

Mmoja wa washiriki alijitambulisha kwa jina moja la Kumburu, alisema amekuwa wakiisikia TBS katika vyombo vya habari, hivyo alitaka kufahamu kama inapatikana Dar es Salaam pekee.

Pia, alitaka kujua walivyojipanga kuwafikia wananchi waliopo mbali kama Ruvuma ikizingatiwa wameongezewa majukumu.

Akijibu swali hilo, Ofisa Masoko TBS, Rhoda Mayugu alisema "Tunafurahi kufahamu kwamba Shirika linafahamika kupitia vyombo vya habari kwa kuwa Shirika hutumia njia mbalimbali kuwafikia wananchi ambazo ni kampeni za uelimishaji umma zinazofanyika katika ngazi za wilaya, mitandao ya kijamii, magazeti, redio, televisheni na maonyesho mbalimbali," alisema.



Mtafiti wa mazao ya nafaka kutoka TARI Kanda ya Mashariki, Ismail Ngolinda (kushoto), akitoa maelezo ya kipando cha mbegu ya teknolojia ya kisasa ya mahindi ambayo imeonyesha mafanikio ya kupambana na wadudu kama viwavi jeshi na kuongeza uzalishaji na tija hadi magunia 30 kwa hekta kwa baadhi ya wakulima na watafiti waliotembelea katika maonyesho hayo ya nane katika viwanja vya Mwalimu J.K Nyerere, Morogoro. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# 2021 ukatili kupunguzwa kwa 50%

**Na Yasmine Protace**

SERIKALI imeandaa mpango wa kitaifa kwa kutekeleza kupunguza ukatili wa kijinsia kwa asilimia 50, ifikapo mwaka 2021.

Hayo yalisemwa na mwakilishi kutoka Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Mwanda, wakati akitoa vyeti kwa washindi wa tuzo za SADC kuhusu masuala ya jenda.

Tuzo hizo zilitolewa katika makundi mbalimbali na washiriki walikuwa waandishi kutoka vyombo mbalimbali katika upande wa Magazeri, Tv, Redio, Blog na makundi yanayojihusisha na masuala ya kijamii katika mambo ya jenda.

Baadhi ya washiriki walishinda tuzo ambazo zinazungumzia jenda na wataiwakilisha Tanzania nchini Afrika Kusini kushindana na nchi zingine ambazo zipo katika umoja wa SADC.

"Gender Link na wenyeji wenu TGNP Mtandao, mmefanya kitu kizuri kwa nchi na kitasaidia kuwaelimisha wananchi katika masuala ya kuzijua haki zao katika usawa wa kijinsia," alisema.

Aliongeza kuwa washiriki waliofanikiwa kushinda wakienda nchini Afrika Kusini wazidi kuzungumzia mafanikio na mikakati iliyowekwa na serikali katika kupambana na masuala ya ukatili.

Pia aliwapongeza washiriki wa mwaka jana waliosaidia kuitangaza Tanzania kupitia mikakati ya kupambana na masuala ya ukatili na hali hiyo ikasaidia Tanzania kuongoza kwa kufanya vizuri kwa kuzungumzia mambo ya jenda ikifuatiwa na Malawi.

Alisema Tanzania inatambua usawa wa kijinsia ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Vile vile alisema wameweka miaka mitano ya kimaendeleo kwa kuwa na sera ya wazee, watoto wenye ulemavu na jamii.

Aliongeza kuwa Tanzania imechagua vitu vitano katika makubaliano ya Beijing na kusimamia uwezeshaji kiuchumi wanawake na ajira.

Vile vile, serikali imeandaa mpango wa kitaifa wa utekelezaji kupunguza ukatili wa kijinsia ifikapo 2021 kwa kwa asilimia 50.

"Vituo 10 vimeanzishwa vya mkono kwa kutatua matukio ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Alisema serikali imetenga asilimia 10 kwa ajili ya kuwawezesha wanawake na vijana.

# TARI yavutia wakulima teknolojia ya mbegu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BANDA la Taasisi ya Kilimo Kanda ya Mashariki (TARI) limekuwa kivutio kikubwa katika maonyesho ya kilimo na mifugo maarufu kama Nanenane, kutokana na kutembelewa na makundi ya wakulima wengi ili kupata elimu ya teknolojia za mbegu zenye uwezo wa kupambana na magonjwa na wadudu aina ya viwavi jeshi pamoja na kuongeza uzalishaji wenye kuleta tija.

Katika maonyesho hayo ya Kanda ya Mashariki yanayofanyika katika Kiwanja cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, yanayohusisha mikoa wa Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Tanga, makundi ya wakulima kutoka mikoa hiyo yamekuwa wakimiminika kujionea vipando vya mazao mbalimbali ambayo yamewekewa mkakati na serikali.

Akizungumzia maonyesho hayo, Mkurugenzi wa TARI Kanda ya Mashariki, Dk. Joel Meriyo, alisema kuwa vipando vilivyopo katika banda lao mwaka huu vimelenga kumuongezea mkulima kutoka uzalishaji wa mazoea na kumpeleka katika uzalishaji wenye tija kwa kutumia mbegu za teknolojia ya kisiasa zenye ukindhani na magonjwa ambayo yamekuwa yakiwasumbua wakulima likiwamo tatizo la viwavi jeshi.

Dk. Meriyo alisema katika vipando vilivyopo kwenye banda la TARI, ni pamoja na mazao ya nafaka ambayo ni mahindi, mtama, mpunga, uwele, mazao ya mafuta kama alizeti, nazi na ufuta, mazao ya mikundekunde ambayo ni choroko, mbaazi maharagwe na dengu, pamoja na miwa, pamba, mihogo, viazi na mboga mboga.

Alisema kuwa TARI imejipanga kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima wote wanaendelea kulitembelea banda hilo katika maonyesho hayo, kutokana na wakulima wengi kuzalisha kwa mazoea bila kuleta tija wakati kuna mbegu za kisasa zilizoboreshwa na kuongeza tija kama ya mahindi na mtama ambazo zinauwezo wa kutoa mpaka magunia 30 kwa hekta moja huku zikileta ukindhani na wadudu.

"Maonyesho ya wakulima ya hivi sasa, sisi kama TARI Kanda ya Mashariki, tumejipanga vyema kupitia watafiti wetu kuwabadilisha wakulima ili kulima kilimo chenye tija na kuongeza uzalishaji maradufu, hakuna sababu ya wao kuwa masikini zipo mbegu za kisasa na zinaongeza uzalishaji na zinapambana na magonjwa ambayo ni changamoto kubwa kwao tunawataka waendelee kuja," alisema.

Kwa upande wake mtafiti wa mazao ya mahindi, mtama na uwele, Ismail Ngolinda, alisema kuwa wamekuja na mbegu mpya za mazao hayo kwaajili ya kutoa

## Trump ashutumiwa kwa matamshi ya ubaguzi

**WASHINGTON, Marekani**

SPIKA wa Chama cha Democrats nchini Marekani, Nancy pelosi, amemshutumu Rais Donald Trump kwa kuishambulia Wilaya ya Baltimore yenye wakazi wengi weusi kuwa eneo lililojaa panya wengi.

Rais Trump alimshambulia mbunge Elijah Cummings na Wilaya ya Maryland katika mtandao wa twitter.

Rais Trump alitaja Wilaya ya Cummings yenye raia wengi weusi - Baltimore kama iliovamiwa na panya.

Rais Trump aliandika kuwa: "Cummings ni mnyanyasaji akikosoa jinsi wahamiaji walipo katika mpaka wa Marekani na Mexico walivyopata shida".

Pelosi aliwaongoza wabunge wa Democrats katika kumtetea Cummings akiyashutumu machapisho ya Rais Trump katika mtandao wake wa twitter.

Machapisho yalioandikwa dhidi ya Cummings ambaye asilimia 50 ya wakazi wa wilaya yake ni weusi kulingana na data ya idadi ya watu nchini Marekani.

Matamshi ya Rais Trump yanajiri wiki chache tu baada ya kukosolewa kwa chapisho jingine la twitter akiwaambia wanawake wa chama cha Congress kurudi wanakotoka.

Ujumbe huo uliwalenga wabunge weusi akiwamo Alexandria Ocasio-Cotez, Rashida Tlaib, Ayanna Pressley na Ilhan Omar - wote wakiwa raia wa Marekani.

Wiki iliopita Cummings alimshutumu Kaimu Katibu wa Usalama, Kevin McAleenan na hali ilivyo katika vituo vya mipakani katika mkutano mmoja wa bunge.

Katika majibizano McAleenan , Cummings alitaka hali kuimarishwa katika vituo hivyo.

Cummings ambaye anawakilisha wilaya ya Maryland alisema kwamba utawala wa Rais Trump hauna huruma katika kuwakabili wahamiaji .

Akichapisha katika mtandao wa twitter siku ya Jumapili, Rais Trump alionekana kukasirishwa na matamshi ya Cummings.

Ujumbe huo wa twitter unajiri siku chache tu baada ya kamati ya Democrats kutaka kujua mawasiliano ya kisiri ya maofisa wandamizi wa Ikulu ya Whitehouse.

Cummings aliushutumu utawala wa Rais Trump kwa kutoweka rekodi za mawasiliano yake kulingana na sheria.

Kamati hiyo ya uchunguzi ni miongoni mwa zinazofuatiliwa na bunge la Democrats katika utawala wa Rais Trump.

Akiwa mkosoaji mkubwa wa Rais Trump, Cummings alisema "ni haki yangu ya kikatiba kuufanyia uangalizi uongozi wako. Na pia ni jukumu langu la kuwapigania watu wangu"

**BBC**

# Watu 700 wauawa ndani ya miezi sita

**KINSHASA, Congo**

MASHIRIKA ya kutetea haki za binadamu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) pamoja na yale ya kimataifa, yametoa wito kwa Serikali kuhakikisha watu waliohusika na utekelezaji wa vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu wanapatikana na kushtakiwa.

Matamshi ya mashirika hayo yamekuja baada ya Umoja wa Mataifa (UN) kutoa ripoti kuhusu haki za binadamu ikionesha kuwa watu zaidi ya 700 nchini DRC ni waathirika wa vitendo hivyo vilivyotekelezwa kati ya Januari hadi Juni mwaka huu.

UN imeeleza kuwa vyombo vya usalama nchini humo vilihusika na mauaji ya watu karibu 245 huku makundi ya waasi yakihusika na mauaji ya watu zaidi ya 418.

Hayo yanajiri wakati mwanzoni mwa wiki ofisi ya timu ya pamoja ya UN inayohusika na masuala ya haki za binadamu ilisema vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vimepungua nchini DRC licha ya kurekodi matukio elfu tatu kati ya Januari hadi Juni mwaka huu.

Timu hiyo ilieleza kuwa vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu nchini humo vilikuwa vya hali ya juu katika kipindi cha miezi sita tangu Rais Felix Tshisekedi aingie madarakani, lakini hata hivyo vimepungua kwa asilimia nane ukilinganisha na mwaka 2018 katika kipindi hicho hicho.

Wanasiasa kadhaa na baadhi ya maofisa wa ngazi ya juu katika vikosi vya usalama na ulinzi nchini DRC wamewekwa kwenye orodha ya vikwazo vya UN kwa tuhuma za kuhusika na vitendo vya ukiukaji haki za binadamu.

***RFI***



Wanajeshi wa Uingereza kutoka kikosi cha ulinzi wa bahari wa Ulaya katika Ghuba ya Uajemi wakifanya doria. **PICHA: REUTERS**

# Ripoti ya mauaji yazusha maandamano mapya

**KHARTOUM, Sudan**

KAMATI iliyoundwa kufanya uchunguzi wa mauaji Sudan, imesema watu 87 waliuawa na wengine 168 walijeruhiwa wakati vikosi vya usalama viliposhambulia maandamano ya amani katika Mji Mkuu wa Khartoum Juni 3.

Mkuu wa kamati hiyo ya uchunguzi iliyoundwa na Baraza la Mpito la Kijeshi (TMC), Fath al- Rahman Saeed alieleza kuwa ukandamizaji huo ulitokea wakati maofisa wa ngazi ya juu walipokiuka amri iliyotolewa na TMC.

Kwenye ripoti yake, Fath al-Rahman, alisema majenerali wanaongoza nchi hawakutoa amri ya kutawanya maandamano yaliyofanyika Juni 3 na kuwatuhumu askari wa kikosi cha kupambana na fujo (RSF) kwa ajili ya mauaji hayo.

Aliongeza kuwa maofisa nane kutoka kikosi hicho cha RSF walikaidi amri ya kutawanya maandamano ya amani juni 3 katika Mji Mkuu wa Khartoum.

Ingawa Fath al-Rahman hakutoa maelezo ya kina ni jinsi gani uchunguzi utaendelea dhidi ya maafisa hao wanaotuhumiwa.

Alisema vikosi vya usalama vilipewa maagizo ya kutawanya watu eneo la karibu na walikopiga kambi waandamanaji linaloitwa Colombia lakini sio kuvamia na kushambulia kambi hiyo kwa sababu ilikuwa ni alama ya vuguvugu lililochangia kumuondoa kiongozi wa muda mrefu Omar al-Bashir.

Baraza la majenerali linaloiongoza nchi limekuwa likisisitiza kwamba halikutoa amri ya kutawanya umati wa waandamanaji bali lilitoa agizo la operesheni ikiwamo ya RSF na vikosi vingine ya kusafisha eneo la Colombia ambalo wanasema lina shughuli za madawa ya kulevya na ghasia.

"Waliondoa vizuizi, wakafyatua mabomu ya kutoa machozi na kufyatua risasi kiholela na kusababisha mauaji ya waandamanaji na wengine kujeruhiwa na kuchomwa kwa matenti," alisema Fath al-Rahman.

Muungano wa Upinzani wa Uhuru na Mabadiliko (FFC), umeikataa ripoti ya kamati ukisema watu zaidi ya 100 waliuawa na kutaka uchunguzi huru.

Juni 3, mwaka huu askari waliokuwa wamevalia sare za kijeshi walivamia eneo ambalo waandamanaji waliketi hapo kwa muda mrefu nje ya makao makuu ya jeshi na kuanza kuwafyatulia risasi na kuwapiga waandamanaji.

Nalo Shirikisho la Wanataaluma wa Sudan (SPA), limekataa uchunguzi huo likisema: "Uliagizwa na baraza la kijeshi lenyewe, na hii inatoa doa uadilifu wake kwa sababu jeshi linatuhumiwa katika kesi hiyo"

Waandamanaji waliojawa na ghadhabu waliandamana siku ya Jumamosi wakiikataa idadi iliyotolewa kama anavyosema mwandamanaji mmoja Amam al-Tahir: "Uchunguzi huu hauna maana kwasababu tunafahamu kilichotokea dhidi ya waandamanaji".

***DW***

## 'Miradi mikubwa iwaongezee ujuzi wahandisi wazawa'

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imeshauriwa kuwekeza katika miradi mikubwa ya ujenzi wa reli ya kisasa na flyover inayotekelezwa nchini kwa kuhakikisha inatumika kuwaongezea ujuzi wahandisi wazawa na wanafunzi wa fani za ujenzi.

Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Wahandisi, Ipyana Moses alitoa ushauri huo jana alipozungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya kutembelea taasisi ya Dar es Salaam Institute of Technology (DIT), mwishoni mwa wiki iliyopita.

Moses alisema taasisi yao imebaini ushiriki mdogo wa wahandisi wazawa kwenye miradi hiyo, hivyo wamewasiliana na serikali na kuishauri kuona jinsi inavyoweza kubadilisha sera kwenye mikataba ya awali ili kubainisha nafasi za wahandisi Watanzania.

"Wahandisi Watanzania wanapaswa kuwekewa nafasi ya kushiriki moja kwa moja kwenye miradi hii mikubwa, ikiwezekana bajeti iwe inaongezwa kidogo kuwawezesha, ili waweze kuwa na bidii ya kujifunza itakayosaidia kuongeza ujuzi wao hivyo kuwajengea uzoefu," Moses alisema.

"Wenzetu madaktari mafunzo yao ya vitendo ni kwenye hospitali, kwa hiyo kwetu sisi ushiriki kwenye miradi kama hii ndiyo sehemu ya kujifunza zaidi," alisema. Alisema taasisi yao ina jukumu la kuwaunganisha wahandisi wote nchini wanajifunza na kushauri cha kufanya ili kumudu kwenye soko, pia kutimiza lengo la kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda.

Akizungumzia ziara hiyo alisema ni sehemu ya utaratibu wa kutembelea shule za sekondari kuhamasisha wananafunzi kupenda masomo ya sayansi, pia kutembelea taasisi zinazotoa mafunzo ya sayansi na uhandisi ili kushauri na kuboresha maeneo ambayo wanabaini kuna udhaifu, hatua ambayo inalenga kuhakikisha wanaohitimu masomo hayo wanakuwa bora.

Mhandisi mshauri wa masuala ya ujenzi wa nyumba na barabara, Erasto Machume, alisema wataalam wa ujenzi wa barabara wao tatizo ni vitendea kazi na uzoefu katika baadhi ya miradi, kwa Tanzania Fly Over ya kwanza ni Mfugale. Mratibu wa ziara hiyo, Dk. John Msuma, alisema hawawezi kuwa na mafanikio bila kuwa na ushirikiano mzuri na wadau, kama taasisi hiyo ambayo tayari ina wahandisi waliopo kwenye soko, hivyo wanatambua zaidi mahitaji yalivyo.

Kaimu Makamu Mkuu wa DIT, Profesa Patrick Nsimama, alisema Taasisi ya Wahandisi ni kubwa na ya kipekee inayounganisha waandaaji wa sera na wasimamizi, wanasayansi, wanateknolojia na wahandisi.

"Hapa watatembelea karakana zote za taasisi zetu baada ya hapo watakuwa na nafasi nzuri ya kutushauri, mahali ambapo wameona kuna maboresho yanahitajika," alisema.

Profesa Nsimama alisema DIT ni taasisi yenye nia ya kuongoza katika kuhakikisha inazalisha wahandisi bora kufanikisha Tanzania ya viwanda vyenye ubora.



# Agnes Sikitu Kabigi ujue umetuvuruga wenzio

AGGIE, zilipoanza fununu za taarifa hizi tulidhani ni tango pori.

Lilian alipotuthibitishia hapa kwamba 'its true', bado hatukutaka kuamini. Si unamjua Lilian bwana, huwa mtundu fulani wa chini chini.

Lakini afadhali Lilian, hivi kwa mfano angekuwa ni Tuma ndiyo kathibitisha, hata kama ni wewe Aggie ungeamini! Maneno ya Tuma si unayajua? Uzuri mafariki wanajuana bwana.

Utani kando, Aggie leo ni siku ya nne tangu kuanza kusikika kwa taarifa hizi hebu tuambie ukweli nini kimekusibu? Unajua Aggie, kutunyamazia siyo vizuri rafiki! Kwani tumekukosea nini? Si useme ili tukuombe msamaha yaishe, maisha yaendelee?

Si kitu, si ni wewe kila wakati unatuambia rafiki ni bora kuliko mwanasesere, kwanini sasa umetufanya hivi? Je, tumekuwa wanasesere siyo marafiki tena? Hapana bwana, hatukubali.

Unajua nini, Jane kaposti ile picha ya mtoko wenu wa majuzi, kama kawa tabasamu lako bwana, eti na glasi mkononi yenye kakitu ndani yake! Huwa nakwambia unapenda kutabasamu kwa sababu una meno meupe, yangekuwa kama ya Jacgueline Liana, thubutu! Utafumba kinywa hadi kinuke.

Jane alivyoposti hiyo picha kwa lengo la kutudolishia tena, ni kama vile Lilian akaona wivu bwana, si akatupia picha ya harusi yako na JB, yaani hiyo ndiyo ikathibitisha hizi habari ni tango pori.

Nikajiuliza hivi Aggie anamuachaje JB kwa mfano! Ulivyomkumbatia na tabasamu lako kama kawa, unamuachaje achaje? Kutoka kote Kenya halafu ndiyo yanakuwa haya!

Aggie mtoto wa Mary Kabigi, nimekumbuka siku ya harusi uliapa kwamba utakuwa na JB kwa shida na raha hadi kifo kitapowatenganisha. Ona sasa kifo kimefanya vitu vyake!

Jana nikaingia humu, Aggie huwezi amini, eti umo ndani ya jeneza huko Shinyanga, nikajisemea kimoyo moyo these guys are kidding! Yaani wanazidi kuendeleza matango pori!

Hapana bwana Aggie, kwa sababu hutaki kusema kilichokusibu, hizi habari siyo bure, umelala kwenye jeneza eeeee, sawa rafiki.

Aggie wenzeio tunalia sana. Tumeumia mno. We are speechless wenzako, kama alivyosema Usia na Jane. Yaani you have gone like a chandle in the wind!

Aggie msalimie mama na kaka Nico. Mwambie mama tumekuwa watu wazima kwa sasa. Tumekuwa wadada wa nguvu. Tumepunguza kwenda kweye majumba ya starehe kunywa na kucheza muziki mpaka chini, mpaka asubuhi.

Usiache kumwambia kwamba kulipangwa mtoko wa nguvu kwenda Tanga, lakini ni wewe na da' Bite ndiyo mlisababisha uahirishwe hadi muwepo.

Oh, kifo kimeutibua kabisa mtoko mbaya mbovu! Jovina aliupania tena baadhi yetu walishaandaa na uongo wa kuwaaga mabosi wao ili wasikose mtoko.

Hebu Sikitu niambie, ni bosi gani unamuomba ruhusa ya mtoko akakuruhusu?

Yaani na imagine Usia aende kwa mabosi wake akaseme hivi "excuse me madame, am asking for permition to travel to Tanga to have fun with friends," atakatwa jicho hilo!

Unajua Aggie, kinachoendelea ni kwamba kesho ndiyo itakuwa siku ya uthibitisho wa habari hizi ambazo Lilian alituthibitishia. Kina Tomaso wanataka kuona, siyo kusikia tu.

Nimekumbuka, Aggie, jana Neli Msuya kanipigia simu kaniambia bado anaona taarifa hizi ni tango pori.

David Kirway vilevile, nilipompa hizi taarifa akaniambia niache utani mbaya. Siyo vizuri.

Yule rafiki yetu Raphael mrefuu, Jane anamfahamu nilivyozungumza naye he did not believe!

Aggie, kwenye magrupu mengine huwezi amini, umekuwa gumzo kubwa! Umesikitisha na kuumiza wengi! Hakuna anayeamini.

Agnes Sikitu Kabigi, ulivyozinduka kidogo baada ya kuanguka, uliwauliza waliokuzunguka, uliwauliza waliokuzunguka kukusaidia kwamba "Nini kimetokea".

Aggie, kuuliza wengine swali hilo ni kuwaonea!

Aggie sisi marafiki zako tunataka jibu tunakuuliza "Aggie, nini kimetokea?"

***Aggie bye!***
***Jackie Liana***

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA CHETI



**Nasra Habib Ndassiwa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S342/0039** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1998 katika shule ya sekondari Shaaban Robert . Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Taifa. Polisi Taarifa: **CD/IR/RB/2366/2008**

115345102

### Eneo la biashara (Yard Plot) mita za Mraba 2,723 linauzwa.

Eneo (yard) Lina hati miliki, Kuna maji na umeme pia.

Eneo lipo Msamvu Morogoro, kandokando ya barabara ya Iringa, karibu na BM Garage

Eneo linafaa kwa matumizi ya kiwanda, maegesho ya malori, Hoteli, Hostel, maofisi, maghala n.k,

Kwa mawasiliano:
godlisten.minja@greenresources.no
+255 714 432 979

215338701


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe

kila siku Tupigie 0767 223 311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe **29/7/2019** kampuni ya **SUMMER COMMUNICATION CO. LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SONGEA** kuelekea **NJOMBE,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 688 CDH/ T 102 CWK**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 17.5 |
| Upana | - | mita | 3 |
| Kimo | - | mita | 4.6 |

3. Njia itakayotumika: **NJOMBE ROAD**
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115345302


NIPASHE

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

EXIM AT WORK TODAY FOR TOMORROW

# "EXIM KAZINI, LEO, KWA AJILI YA KESHO"

EXIM AT WORK TODAY FOR TOMORROW

## EXIM BANK (TANZANIA) UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA AMBAZO ZIMEKAGULIWA

Imetolewa chini ya Kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya mwaka 2014

**Fedha za Wanahisa**
@ Bilioni 174

**Jumla ya Mali**
@ Trilioni 1.68

**Amana za Wateja**
@ Trilioni 1.23

**Matawi**
@ 46

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | KAMPUNI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | KUNDI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | KAMPUNI ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2019 | KUNDI ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2019 |
|---|---|---|---|---|
| **MALI** | | | | |
| 1 Fedha Taslimu | 18,078 | 30,973 | 16,709 | 31,544 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 80,005 | 141,136 | 47,458 | 107,136 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 233,726 | 240,709 | 235,175 | 242,658 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 43,527 | 99,781 | 14,216 | 63,642 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 1,447 | 3,062 | - | 2,288 |
| 6 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 89,434 | 91,898 | 29,615 | 55,587 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyigine | 7,381 | 26,841 | 7,378 | 862 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 667,818 | 922,597 | 671,374 | 911,831 |
| 12 Mali nyingine | 48,986 | 56,352 | 40,679 | 44,742 |
| 13 Uwekezaji katika Hisa | 33,128 | 1,254 | 34,083 | 2,208 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 34,815 | 44,142 | 38,859 | 48,017 |
| 16 Mali isiyo ya sasa yanayotumiwa | 15,728 | 17,641 | 15,728 | 17,641 |
| **17 JUMLA YA MALI** | **1,274,071** | **1,676,386** | **1,151,274** | **1,528,156** |
| **B DHIMA** | | | | |
| 18 Amana za Benki na Taasisi za Fedha | 319,838 | 103,533 | 209,132 | 75,742 |
| 19 Amana za Wateja | 648,020 | 1,230,802 | 648,778 | 1,122,036 |
| 20 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| 21 Amana Maalumu | 2,229 | 2,229 | 2,770 | 2,770 |
| 22 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 279 | 279 | 281 | 281 |
| 23 Hundi na Hawala za Kibenki Zilitolewa | 1,511 | 1,969 | 1,531 | 3,934 |
| 24 Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 6,306 | 9,426 | 9,116 | 11,219 |
| 25 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya benki | - | - | - | - |
| 26 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 27 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 1,586 | 1,944 | 1,505 | 1,726 |
| 28 Dhima Nyingine | 11,069 | 31,913 | 16,871 | 35,249 |
| 29 Madeni | 119,417 | 120,117 | 100,696 | 105,328 |
| **30 JUMLA YA DHIMA** | **1,110,255** | **1,502,212** | **990,681** | **1,358,285** |
| **31 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **163,817** | **174,174** | **160,592** | **169,872** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 32 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 12,900 | 12,900 | 12,900 | 12,900 |
| 33 Akiba ya Mtaji | 10,877 | 13,356 | 10,901 | 13,356 |
| 34 Mapato Yaliyobakizwa | 135,452 | 129,654 | 134,651 | 129,587 |
| 35 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 4,588 | 7,725 | 2,141 | 3,423 |
| 36 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - | - | - |
| 37 Stahiki ya Wenye hisa Chache | - | 10,540 | - | 10,607 |
| **38 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **163,817** | **174,174** | **160,592** | **169,872** |
| 39 Dhima Zisizo Dhahiri | 159,543 | 162,524 | 151,683 | 152,144 |
| 40 Mikopo Chechefu | 59,221 | 70,312 | 56,915 | 75,518 |
| 41 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 49,054 | 54,766 | 46,306 | 51,361 |
| 42 Mali Nyingine Chechefu | 6,698 | 6,698 | 5,357 | 5,357 |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.86% | 9.76% | 13.95% | 10.42% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.24% | 7.18% | 7.93% | 7.83% |
| Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74.23% | 73.44% | 83.67% | 80.50% |
| Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 52.42% | 55.03% | 58.32% | 59.67% |
| Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84.38% | 82.50% | 86.15% | 83.55% |
| Ongezeko la Amana | 13.08% | 11.40% | -7.04% | -4.42% |
| Ongezeko la Mali | 10.67% | 9.70% | -4.83% | -2.30% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | KAMPUNI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | KUNDI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | KAMPUNI ROBO MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2018 | KUNDI ROBO MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2018 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2018 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa | | | | | | | | |
| 1 Mapato ya Riba | 26,356 | 34,546 | 24,494 | 31,342 | 49,885 | 64,420 | 50,326 | 63,379 |
| 2 Gharama za Riba | (8,463) | (10,580) | (7,715) | (9,416) | (16,127) | (18,797) | (16,020) | (18,429) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (**1 kutoa 2**) | **17,894** | **23,967** | **16,779** | **21,926** | **33,758** | **45,623** | **34,307** | **44,951** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (220) | (220) | (158) | (158) | (353) | (353) | (12,821) | (12,821) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,716) | (2,686) | (559) | (3,366) | (2,921) | (4,590) | (926) | (5,648) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **7,532** | **13,669** | **9,179** | **13,879** | **17,134** | **26,677** | **19,719** | **26,085** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,921 | 3,151 | 1,552 | 2,910 | 5,434 | 7,960 | 3,031 | 5,585 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,852 | 8,634 | 5,284 | 8,047 | 9,856 | 17,106 | 11,003 | 16,175 |
| 6.3 Gawio | 21 | 21 | 21 | 21 | 21 | 21 | 21 | 21 |
| 6.4 Mapato Mengine | 738 | 1,864 | 2,322 | 2,901 | 1,825 | 1,590 | 5,664 | 4,304 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(20,553)** | **(29,169)** | **(20,769)** | **(28,804)** | **(41,622)** | **(56,542)** | **(40,271)** | **(53,259)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (8,479) | (12,698) | (8,822) | (12,788) | (16,816) | (24,825) | (17,186) | (24,821) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | (445) | 0 | (282) | - | (683) | 0 | (558) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (12,074) | (16,026) | (11,946) | (15,734) | (24,807) | (31,033) | (23,085) | (27,880) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **2,937** | **5,561** | **4,473** | **3,478** | **5,996** | **10,815** | **8** | **(693)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (490) | (1,249) | (1,336) | (1,336) | (1,408) | (3,090) | 4 | (597) |
| 10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 2,447 | 4,313 | 3,138 | 2,142 | 4,588 | 7,725 | 12 | (1,291) |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **2,447** | **4,313** | **3,138** | **2,142** | **4,588** | **7,725** | **12** | **(1,291)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 675 | 970 | 685 | 967 | 675 | 970 | 685 | 967 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 190 | 334 | 243 | 166 | 356 | 599 | 1 | (100) |
| **15 Idadi ya Matawi** | **32** | **46** | **34** | **48** | **32** | **46** | **34** | **48** |
| **VIASHIRIO VYA UTENDAJI** | | | | | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.8% | 1.0% | 1.0% | 0.5% | 0.5% | 0.6% | 0.0% | -0.1% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.3% | 7.1% | 5.8% | 2.9% | 3.3% | 4.3% | 0.0% | -1.7% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 80.8% | 77.5% | 80.0% | 80.4% | 81.8% | 78.2% | 74.5% | 75.0% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.2% | 6.7% | 6.5% | 6.3% | 4.6% | 4.2% | 13.4% | 12.9% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30.06.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | KAMPUNI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | KUNDI ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | KAMPUNI ROBO MWAKA LINGANISHI ILIYOPITA 31.03.2019 | KUNDI ROBO MWAKA LINGANISHI ILIYOPITA 31.03.2019 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2018 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.06.2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 2,937 | 5,561 | 3,058 | 5,264 | 5,996 | 10,815 | 8 | (693) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 4,213 | 1,527 | 3,519 | 1,615 | 7,732 | 1,527 | 5,689 | 6,981 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,556 | (10,766) | (11,504) | (34,758) | (7,948) | (45,524) | 3,409 | (2,137) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | 425 | 425 | 425 | 425 | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 109,407 | 136,558 | (65,183) | (55,350) | 44,223 | 81,208 | (26,054) | 65,741 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | 7,899 | 8,738 | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (9,075) | (4,619) | 855 | 601 | (1,176) | 5,744 | 1,723 | 7,137 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (5,712) | (12,333) | - | - | (4,857) | (11,732) | (3,621) | (6,601) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - | - | - | (2,495) | (2,495) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **105,327** | **115,929** | **(60,931)** | **(73,465)** | **44,395** | **42,464** | **(21,341)** | **67,934** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililopokewa | 21 | - | 425 | (2,649) | 21 | - | 21 | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | 541 | (756) | (425) | (425) | 966 | (3,405) | (2,538) | (1,617) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | (36,334) | (44,794) | (425) | (425) | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 1,446 | (24,031) | - | - | (34,888) | (68,825) | 10,677 | 6,736 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | | | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **2,008** | **(24,786)** | **(36,334)** | **(47,868)** | **(34,327)** | **(72,654)** | **8,159** | **5,119** |
| | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 18,721 | 14,789 | - | - | 19,020 | 19,720 | (10,133) | (10,281) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **18,721** | **14,789** | **299** | **4,931** | **19,020** | **19,720** | **(10,133)** | **(10,281)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 126,055 | 105,932 | **(96,965)** | **(116,402)** | 29,089 | (10,471) | (23,315) | 62,772 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 101,739 | 180,050 | 198,704 | 296,452 | 198,704 | 296,452 | 163,345 | 207,432 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 227,794 | 285,980 | 101,739 | 180,050 | 227,794 | 285,980 | 140,030 | 270,204 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06. 2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| KAMPUNI | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyo bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **135,452** | **4,488** | **6,389** | **-** | **159,229** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 4,588 | - | - | - | 4,588 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho Kipindi kilichoishia 30.06.2019** | **12,900** | **-** | **140,040** | **4,488** | **6,389** | **-** | **163,817** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **158,809** | **35,486** | **6,363** | **54** | **213,612** |
| Mabadiliko ya mwanzo ya IFRS 9 | - | - | (40,321) | - | - | (119) | (40,440) |
| Marekebisho mengine | - | - | 23,705 | (23,705) | (13) | - | (13) |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **12,900** | **-** | **142,193** | **11,781** | **6,350** | **(65)** | **173,159** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (13,995) | - | - | - | (13,995) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 65 | 65 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 7,293 | (7,293) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (39) | - | 39 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | **-** | **135,452** | **4,488** | **6,389** | **-** | **159,229** |
| **KUNDI** | | | | | | | |
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **129,227** | **7,470** | **5,885** | **10,967** | **166,449** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 8,153 | - | - | (427) | 7,725 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho Kipindi kilichoishia 30.06.2019** | **12,900** | **-** | **137,379** | **7,470** | **5,885** | **10,540** | **174,174** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | **-** | **152,685** | **46,457** | **6,447** | **12,965** | **231,454** |
| Mabadiliko ya mwanzo ya IFRS 9 | - | - | (47,668) | (119) | - | (828) | (48,615) |
| Marekebisho mengine | - | - | 23,594 | (23,437) | - | (157) | - |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **12,900** | **-** | **128,611** | **22,901** | **6,447** | **11,980** | **182,839** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (12,380) | - | - | (3,399) | (15,779) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | (562) | - | (562) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | (49) | (49) |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 12,148 | (14,036) | - | 1,888 | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 848 | (1,395) | - | 547 | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | **-** | **129,227** | **7,470** | **5,885** | **10,967** | **166,449** |

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| JAFFARI MATUNDU **Ofisa Mtendaji Mkuu** | ……………………………….. | 26.07.2019 |
| SELEMANI PONDA **Mkuu wa Fedha** | ……………………………….. | 26.07.2019 |
| COLMAN RIWA **Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ……………………………….. | 26.07.2019 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| YOGESH MANEK **MKURUGENZI** | ……………………………….. | 26.07.2019 |
| JUMA MWAPACHU **MKURUGENZI** | ……………………………….. | 26.07.2019 |

215345802

Kwa maelezo zaidi piga simu 080 078 0111 au tembelea www.eximbank.co.tz

EXIM BANK
*Innovation is life*

TANGAZO

# EXIM BANK (TANZANIA) LIMITED MINIMUM DISCLOSURE OF THE BANK CHARGES AND FEES FOR THE SECOND QUARTER 2019

| ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|
| **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| Transaction fee | N/A |
| Monthly service fee ( break down per customer type) | 4,000 |
| Annual Fee (Student Account) | 10,000 |
| Statement | FREE |
| Interim statement | 6,000 |
| Withdrawal Charges at domicile branch | 3,500 |
| Withdrawal Charges over the Counter at non domile branch for non preferred customers | 1.2% of the amount |
| Withdrawal bulky without notice | N/A |
| Cash Deposit Charge at Domicile branch | FREE |
| Cash Deposit Charge at non domicile branch by non preferred customers | FREE |
| Savings Card/Passbook | N/A |
| Passbook/Card Replacement | N/A |
| Coin Deposit Fee | 12% of the amount |
| Closing Account | FREE |
| | |
| **CURRENT ACCOUNT** | |
| Monthly service fee (break down per customer type) | 18,000 |
| Transaction fee | N/A |
| Statement | FREE |
| Interim statement | 6,000 |
| Periodic Schedule Statement | N/A |
| Withdrawal Charges at domicile branch | 1,200 for amount up to 20mns,0.12% above subject at maximum of 125,000 |
| Withdrawal Charges over the Counter at non domile branch for non preferred customers | 1.2% of amount |
| Cash Deposit Charge at domicile branch | FREE |
| Cash Deposit Charge at non domicile branch by non preferred customers | FREE |
| Coin Deposit Fee | 12% of the amount |
| Closing Account | FREE |
| Deposit fee | N/A |
| Bank Drafts | N/A |
| Bank Drafts cancellation charge | N/A |
| Cheque book | 60,000 for 100 leaves and 42,000 for 50 leaves |
| Cash Withdrawal at Counter | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject to maximum of 125,000 |
| Special Clearance | N/A |
| Cheque withdraw over the counter | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject to maximum of 125,000 |
| Dishonoured cheque | 30,000 |
| Cash Payment to 3rd party | FREE |
| Cash Deposit Charge | 1200 for amount up to 20mns,0.12% above subject to maximum of 125,000 |
| Overdrawn account interest charge | 27% of the amount overdrawn |
| Unarranged Overdraft | N/A |
| Bulk cash Deposit | N/A |
| Bulk cash Withdrawal | N/A |
| Stop Payment orders | 42,000 |
| Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| Standing Orders ( to other bank) | 30000 + Tiss charges |
| Certificate of Balance | 15,000 |
| Letter of introduction | FREE |
| Salary handling | FREE |
| School fees deposits | FREE |
| TRA collection | FREE |
| Safe custody charges | Small: 180,000 Medium:270,000 Large:720,000 and Extra large 840,000 p.a |
| Safe custody access fees | FREE |
| **EFT** | |
| Within the same bank (On Us) | 1,200 |
| To other Banks ( On Others) | 1,200 |
| | |
| Outward Transfers | USD 60 |
| Inward foreing Transfers(foreing inward remittances) | USD 6 for receipt up to USD 10k AND USD 12 for receipt above USD 10K |
| | |
| Within the same bank (On Us) | FREE |
| To other Banks ( On Others) | 10,000 per entry |
| **FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT** | **Savings Acc** |
| Transaction fee | N/A |
| Statement | FREE |
| Interim statement | N/A |
| Withdrawal Charges at domicile branch | 1.44% of amount |
| Withdrawal Charge of Low denomination notes of (20,10,5, and 1) | FREE |
| Withdrawal Charges over the Counter at non domile branch for non preferred customers | 2.4% of amount |
| Cash Deposit Charge at domicile branch | 12% for small Denominations (1,5,10,20) only |
| Cash Deposit Charge at non domicile branch by non preferred customers | FREE |
| Cash Deposit charge of low denomination notes of (20,10,5, and 1) | 12% of amount |
| Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A |
| Purchase of Foreign Cheque | N/A |
| Sale/ Purchase of cash passport | N/A |
| Telex/SWIFT | N/A |
| Transfer from foreign currency denominated account to local account | FREE |
| Outward foreign transfers | 60USD/42GBP/42EUR/600ZAR |
| Inward foreign transfers - Customers | |
| LC Opening/ Advising commision (cash covered) | 1.8% p.a (Negotiable for large amounts) Min $600+$240 swift charges |
| LC Opening/ Advising commision (No cash covered) | 180 USD |
| LC Acceptance commission | N/A |
| LC Payment/settlement commision | N/A |
| LC Amendments | 120 USD |
| Others | NIL |

**ATM TRANSACTIONS**

| | |
|---|---|
| Local Cards | |
| Issue of ATM card | N/A |
| Replacement ATM Card (Faulty) | N/A |
| Replacement ATM Card (Lost) | N/A |

| | |
|---|---|
| **International Cards** | |
| Issue of ATM card | FREE |
| Issue of Prepaid Card | Tzs 10,000 |
| Balance Inquiry – onus ATM | Tzs 240 |
| Balance Inquiry – Remote onus ATM | Tzs 600 |
| PIN regeneration | Tzs 6600 |
| ATM card replacement (Faulty/Lost) | Tzs 19000 |
| EMV Annual fee | Tzs 2,000/ 1000 (Student EMV fee) per month |

| | |
|---|---|
| **ATM WITHDRAWALS:** | |
| **ATM Withdrawals:** | |
| Within the same bank (On Us) | 1,200 per transaction |
| To other banks ATM (On others) | 3.6% of withdrawal, Min Tsh 2,200 |
| ATM mini statement | 400 |
| Bill payments through ATM | N/A |
| **POS** | |
| Within the same bank (On Us) | FREE |
| To other banks ATM (On others) | FREE |
| **MOBILE (SMS) BANKING** | |
| Balance Inquiry | 240 |
| Payments | As per service provider tariff |
| Transfers | Tzs 1,200-Tzs 6,000 |
| | |
| Mini Statement | 240 |
| **INTERNET BANKING** | |
| Domestic: | N/A |
| Balance Inquiry | N/A |
| Payments | N/A |
| **International** | |
| Balance Inquiry | 7,200 per annum |
| Payments | Tsh 600 per month for Individual & Tsh 15,000 per month for Corporate |
| Transfers | Token Fee of Tsh 100,000 |
| **Money Remittances** | |
| Western Union | N/A |
| Sending | N/A |
| Received | N/A |
| **Money Gram** | |
| Inward | FREE |
| Outward | As per Moneygram tariff |
| **Coinstar** | |
| Inward | N/A |
| Outward | N/A |
| **Travelex** | |
| Inward | N/A |
| Outward | N/A |
| **Africash** | |
| Inward | N/A |
| Outward | N/A |
| **Others (Specify)** | |
| Inward | NIL |
| Outward | NIL |

**INDICATIVE FIXED DEPOSIT RATES**

TZS INDICATIVE FIXED DEPOSIT RATES (% p.a.)

| Amount | 30 - less than 90 days | 90 days and < 180 days | 180 days and < 1 yr | 1 yr and < 2 yrs | 2 years and above |
|---|---|---|---|---|---|
| <100m | 2.50% | 4.00% | 5.50% | 7.50% | 8.00% |
| 100m-500m | 3.00% | 4.50% | 6.00% | 7.75% | 8.25% |
| 500m-1bn | 3.50% | 4.50% | 6.25% | 7.75% | 8.25% |
| 1bn and above | 4.25% | 4.50% | 6.25% | 8.00% | 8.25% |

USD FIXED DEPOSIT RATES (% p.a.)

| Amount | 30 - less than 90 days | 90 days and < 180 days | 180 days and < 1 yr | 1 yr and < 2 yrs | 2 years and above |
|---|---|---|---|---|---|
| <100m | 0.50% | 1.00% | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 100k-500k | 0.75% | 1.50% | 2.00% | 3.25% | 3.50% |
| 500k-1m | 1.50% | 1.75% | 2.50% | 3.50% | 3.50% |
| 1m and above | 1.75% | 2.50% | 3.00% | 3.75% | 3.75% |

EUR/GBP FIXED DEPOSIT RATES (%p.a)

| Amount | 30 - less than 90 days | 90 days and < 180 days | 180 days and < 1 yr | 1 yr and < 2 yrs | 2 years and above |
|---|---|---|---|---|---|
| <100k | 0.25% | 0.50% | 0.75% | 1.00% | 1.00% |
| 100k-500k | 0.50% | 0.75% | 1.00% | 1.25% | 1.25% |
| 500k-1m | 0.75% | 1.00% | 1.25% | 1.50% | 1.50% |
| 1m and above | 1.00% | 1.25% | 1.50% | 1.75% | 1.75% |

| LOANS | |
|---|---|
| (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 2.70% |
| (i) Personal loans | 24% TZS 10$ USD |
| (ii) Overdrafts | 19% TZS and 10% USD |
| (iii) Mortgage finance | 20% TZS 10% USD |
| (iv) Asset finance | 9%USD -19%TZS |
| (b) Unpaid loan instalment | 27%pa for local curreny and 14.5.% p.a for USD |
| (c) Early repayment | 5% pa for mortgage loan vs 5% pa for personal and vehicle loan |
| (d) Valuation fees | As per Valuer |
| (e) Other | N/A |

*Mark up is 4% on international transactions

The Bank was penalised Tshs 5 million for failure to comply with Guideline on sorting, counting, packaging cash depositing and counterfeits detection for the quarter ended 30th June 2019. We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| NAME AND TITLE | SIGNATURE | DATE |
|---|---|---|
| JAFFARI MATUNDU<br>CHIEF EXECUTIVE OFFICER | | 26TH JULY 2019 |
| SELEMANI AMAN PONDA<br>CHIEF FINANCE OFFICER | | 26TH JULY 2019 |
| COLMAN S. RIWA<br>CHIEF INTERNAL AUDITOR | | 26TH JULY 2019 |

215345802

EXIM AT WORK TODAY FOR TOMORROW

For more details call 080 078 0111 or visit www.eximbank.co.tz

EXIM BANK
Innovation is life

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL YAKARIBIA KUMSAJILI PEPE

Yakubali kulipa euro milioni 80, lakini kwa mafungu...

**LONDON, England**

ARSENAL inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Lille, Nicolas Pepe ndani ya saa 24 baada ya kukubaliana ada yake ya uhamisho ya euro milioni 80 ambayo italipwa kwa mafungu.

Wiki iliyopita iliripotiwa kwamba, klabu kadhaa zilifikia makubaliano ya kumsajili Pepe kutoka Lille kwa ajili ya msimu mpya ikiwapo klabu ya Ligi Kuu England, Manchester United na Liverpool, pamoja na miamba wa Italia, Napoli zikimwania nyota huyo.

Usajili wa Pepe umekuwa ukipamba vyombo vya habari, lakini mwandishi wa michezo wa Italia, Fabrizio Romano ameripoti kuwa Arsenal ndiye sehemu ambayo atacheza mshambuliaji huyo msimu huu.

Kwa mujibu wa mwandishi huyo, usajili huo utakamilika ndani ya saa 24 kutoka sasa.

Arsenal watalipa kiasi hicho cha euro milioni 80 kwa ajili ya huduma ya Pepe, lakini kwa awamu tofauti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amepewa ofa ya kusaini mkataba wa miaka mitano na klabu yake imefikia makubaliano licha ya Napoli kuripotiwa kwamba wanataka kutuma ofa nyingine.

Awali ilionekana kama Arsenal wangeachana na mpango wao wa kumsajili Pépé na kuelekeza nguvu zao kumtaka Wilfried Zaha kutoka Crystal Palace, lakini timu hiyo imekataa ofa kutoka kwa washikabunduki hao.

Arsenal imeripotiwa kuwa msimu huu imepewa bajeti ya pauni milioni 40 pekee kwa ajili ya kufanya usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Hadi sasa Arsenal imekamilisha usajili wa William Saliba na Dani Ceballos ambaye ametua hapo kwa mkopo.

## KWA UFUPI

**CITY, UNITED KIMYA**

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers, amesema kuwa bado hawajapokea ofa yoyote rasmi ya kumuuza beki wa Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, licha ya kuwapo na tetesi za kutakiwa na Manchester United na Manchester City, akiongeza kwamba klabu pamoja na beki huyo wote hawana hofu juu ya uhamisho huo. ***(Leicester Mercury)***

**FERNANDES MAMBO SAFI**

MANCHESTER United iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes (24), ambaye dau lake limetajwa kuwa ni Euro milioni 70. ***(Sport - in Spanish)***

**DYBALA: NATAKA KUBAKI JUVE**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala (25), amesema kuwa anataka kubakia Juventus na anajiandaa kupambana kutafuta namba katika kikosi cha Maurizio Sarri. ***(Sky Sports)***

**FERGUSON AMTAKA MCGINN**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, anaitaka klabu hiyo kumsajili kiungo wa Aston Villa, raia wa Scoland, John McGinn - ambaye babu yake yuko karibu na kocha huyo. ***(Sun)***

**BALE AELEKEA CHINA**

WINGA wa Wales na Real Madrid, Gareth Bale (30), atakuwa analipwa kiasi cha mshahara wa pauni milioni 1.1 kwa mwaka na mshindani wake, Lionel Messi ataendelea kubakia kuwa nyota ghali baada ya kukubali kujiunga na Jiangsu Suning inayoshiriki Ligi Kuu China kwa mkataba wa miaka mitatu. ***(Express)***

**MADRID MTEGONI**

REAL Madrid itapata hasara ya pauni milioni 86 katika usajili wa Gareth Bale kama mchakato wa uhamisho wa kuelekea Jiangsu Suning hautakuwa umekamilika hadi kufikia siku ya mwisho ya dirisha za usajili la China kufungwa. Klabu hiyo imekubali kulipa dau la usajili ambalo litaendelea kuweka rekodi kwa nyota huyo wa Wales. ***(Mail)***

**POGBA BADO SOKONI**

MABOSI wa Real Madrid watakuwa tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 150 ili kumsajili kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26), baada ya kufanikisha kumuuza Gareth Bale. (Sun)

**NEWCASTLE YABANWA**

NEWCASTLE United haiko tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 20 kwa Hull City ili kumsajili mshambuliaji, Jarrod Bowen, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Newcastle Chronicle)***

**MC CARTHY ANUKIA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle United inajipanga kutoa kiasi cha pauni milioni 5 ili kumnasa kiungo, James McCarthy (28), ambaye hana nafasi katika kikosi cha Everton. ***(Sun)***

**GUEYE MAMBO BADO**

KOCHA wa Everton, Marco Silva anasisitiza kuwa bado mabingwa wa Ufaransa, Paris St-Germain hawajakamilisha mchakato wa usajili wa kiungo wa Senegal, Idrissa Gueye (29), na kocha huyo Mreno anaamini mchezaji huyo atabakia Goodison Park. ***(Liverpool Echo)***

**GUEYE AIKATAA UNITED**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Senegal, Idrissa Gueye, alitarajiwa kutua jijini Paris, Ufaransa jana kwa ajili ya kufanya vipimo vya afya baada ya kukataa ofa iliyowasilishwa na Manchester United. ***(Express)***

**WOLVES, MILAN SAFI**

WOLVES imefikia makubaliano na AC Milan kwa ajili ya uhamisho wa straika, Patrick Cutrone (21). Klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England inataka kumsajili Mtaliano huyo kujiunga na Molineux. ***(Express and Star)***

**HODGSON AMTAKA ANTONIO**

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, anajiandaa kumsajili mchezaji kiraka wa West Ham, Michail Antonio, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

**HABARI MICHEZO**

# TAWI LA YANGA LAIPIGA TAFU HOSPITALI YA MWANANYAMALA

**Na Mwandishi Wetu**

WANACHAMA wa Yanga wa Tawi la nguvu ya Buku lenye makazi yake Mwananyamala jijini Dar es Salaam, jana walikabidhi rasmi msaada wa ukarabati wa Wodi ya Wanaume namba 5, ikiwa ni kuelekea kilele cha siku ya Wananchi itakayofanyika Agosti 4 mwaka huu.

Akizungumza na wanahabari mara baada ya makabidhiano hayo, mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mwananyamala, Mussa Wambura, aliwapongeza Wanayanga tawi la Nguvu ya Buku kwa fikra za msaada walioufikiria na fundisho tosha kwa wengine.

**Wambura alisema kitendo walichokifanya kitabaki kuwa historia kwa Hospitali ya Mwananyamala na kuwaomba jamii ziige kutoa misaada ya namna hii inayomgusa kila binadamu.**

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Sindano Mwananyamala ambako Tawi hilo linapatikana aliwapongeza wanachama hao kwa kitendo hiko cha kijamii.

Nae Mwenyekiti wa Nguvu ya Buku, Ally Kuacha, aliwapongeza wanachama wake kwa kujitoa mpaka kukamilisha mchakato mzima waliokuwa wamekusudia kuelekea kilele cha siku ya wananchi na kuwaomba waendelee na mshikamano huohuo siku zote.

Katibu wa Tawi la Yanga la Nguvu ya Buku, Juma Iyagala, alisema ukarabati huo wa Wodi ya Wanaume umegharimu Sh. 1,830,000 ambapo ni kupaka rangi ndani na nje, kupaka rangi bati pamoja na kubadilisha nyavu za mbu.




Wanachama wa Yanga wa Tawi la nguvu ya Buku lenye makazi yake Mwananyamala jijini Dar es Salaam wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kutoa msaada kwa hospitali ya Mwananyamala. **PICHA NA MPIGAPICHA WETU.**

# Minziro kujiunga Singida wiki ijayo

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA mkuu wa timu ya Singida United, Filex Minziro, anatarajia kujiunga na kikosi chake Agosti 2 Mwaka huu, akitokea mkoani Kagera ambapo alikwenda kwenye shuhuli za kumuenzi baba yake mzazi.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka Kagera alisema bado anaendelea na majukumu ya familia na kudai programu ndani ya timu yake zinaendelea kama kawaida.

"Mimi sipo na timu nipo Bukoba nimekuja," alisema Minziro.

Alisema amesajili wachezaji wazuri ambao Msimu ujao wataleta ushindani mkubwa ndani ya timu hiyo.

**"Sina shaka na kikosi nilichokisajili kikubwa ni kuwapa mazoezi bila kupumzika tu weze kushika nafasi ya juu kwenye Ligi Kuu,"alisema kocha huyo.**

Hata hivyo Minziro aliongeza kuwa Ligi Kuu Msimu ujao inatarajiwa kuwa ngumu na yenye ushindani kutokana na usajili mzuri uliofanywa na kila timu.

Aliomba mashabiki wake waendelee kuwaunga mkono ili washike nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi hiyo.



# ZFCA yafanya marekebisho ya katiba

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIBU wa chama cha makocha Zanzibar( ZFCA), Ibrahim Makeresa, amesema wamefanya marekebisho ya katiba ya chama hicho ambayo sasa makocha watapata fursa ya kukata rufaa pale wanapoadhibiwa.

Akizungumza na Nipashe, alisema hatua ya kufanya marekebisho imekuja kufuatia agizo la rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar, Seif Kombo Pandu la kuwataka kuwa na katiba hai.

Alisema kuwa marekebisho hayo ya katiba ni ya pili kufanyika ambapo kwa mara ya mwisho yalifanyika mwaka 2012.

Hata hivyo, alisema katika katiba hiyo kuna vitu vimeongezwa na vyingine kupunguzwa kwa maslahi ya chama hicho na makocha kwa ujumla.

Aliyataja mambo waliyoyaongeza ni pamoja na kuwapo kwa kamati ndogo ndogo ikiwamo ya usuluhishi na nidhamu, kuwapo kwa mikoa badala ya kuwa na wilaya pekee, wameingiza sifa za mgombea pamoja na mipaka ya kocha wa kigeni.

Aidha alisema kuwa katika vitu ambavyo wamepunguza ni kuondoa wilaya kuchaguwa mjumbe mmoja kwenda taifa na sasa itakuwa kila mkoa utatoa mjumbe mmoja kwenda taifa.

Alisema kuwa kwa marekebisho hayo yaliyofanywa ndani ya katiba yao hiyo sasa katiba yao itakuwa inakwenda sambamba na katiba ya Shirikisho la Soka.

Aidha alisema licha ya kuwa na viongozi pia watakuwa na wajumbe watano kutoka katika mikoa, jambo ambalo hapo nyuma halikuwepo.

Katiba hiyo ya mwaka 1988 tayari imeshapitishwa na mrajisi na sasa kilichobakia ni saini ya katibu wa Shirikisho la Soka Zanzibar ZFF na baadae itasambazwa katika mikoa yote ya Zanzibar pamoja na wilaya zake.

# Michezo

Jumatatu Julai 29, 2019

Nipashe




## Arsenal yakaribia kumsajili Pepe

HABARI UK 30



Mchezaji wa Taifa Stars, Idd Seleman, akijaribu kumtoka mlinzi wa timu ya taifa ya Kenya kwenye mchezo wa kuwania kufuzu kucheza michuano ya mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) jana, kwenye uwanja wa taifa jijini Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka sare ya bila fungana. **PICHA : MPIGAPICHA WETU.**

# STARS 0 KENYA 0

## ●●●Yalazimishwa sare na Kenya kwenye kufuzu CHAN..

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya taifa ya Tanzania jana ililazimishwa sare ya bila kufungana na Kenya kwenye mchezo wa kuwania kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa Ndani (CHAN), mchezo uliopigwa uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, Stars walionekana kuwa kwenye kiwango bora zaidi katika kipindi cha kwanza, huku wakikosa nafasi nyingi za wazi za kufunga mabao.

Safu ya ushambuliaji ya Stars iliyokuwa ikiongozwa na nahodha wake, John Boko, ilishindwa kutumia nafasi walizopata kufunga mabao.

Hadi kipindi cha kwanza kinamaliza, Stars walionekana kuwa wamefika mara nyingi zaidi langoni mwa Kenya lakini wakashindwa kufunga mabao.

Kipindi cha pili kilianza kwa Kenya kulishambulia zaidi lango la Stars, lakini umahiri wa mabeki Erasto Nyoni na Kelvin Yondani ulisaidia kuepusha hatari za kufungwa.

Hata hivyo, Stars ilionekana kuamka zaidi katika dakika za majeruhi kwa kukosa nafasi kadhaa za wazi, huku wakishambulia kwa kasi.

Sasa Stars italazimika kwenda kutafuta matokeo zaidi nchini Kenya katika mchezo wa marudiano.

Endapo Stars itashinda mechi dhidi ya Kenya itakutana na kati ya timu ya Taifa ya Burundi au Sudan, ikishinda itakuwa imepita katika hatua ya fainali ya michuano hiyo.

Kikosi cha Stars: Juma Kaseja, Paul Godfery, Gadiel Michael, Erasto Nyoni, Kelvin Yondani, Jonas Mkude, Hassan Dilunga, Salum Abobakar, John Bocco, Ayubu Lyanga na Idd Seman.

## Simba kumaliza na Orlando Pirates kesho

**Na Mwandishi Wetu**

SIMBA kesho Jumanne itacheza mchezo wake wa mwisho wa kujipima nguvu dhidi ya timu ya Orlando Pirates ya Johannesburg ya nchini Afrika Kusini ilikoweka kambi ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu na mechi za kimataifa.

Baada ya mchezo huo Simba itarejea nchini kwa kwa ajili ya tamasha la Simba Day litakofanyika Agosti 6 mwaka huu, ambao watamenyana na Power Dynamos ya Zambia ukiwa ni mchezo mwingine wa kirafiki. Simba imelazimika kurudisha nyuma kwa siku mbili tamasha hilo ambalo kila mwaka hufanyika Agosti 8 baada ya ratiba ya Ligi Mabingwa Afrika kutoka ikionyesha mechi za kwanza za raundi ya kwanza zitachezwa kati ya Agosti 9 na 11.

Simba itaanzia ugenini dhidi ya UD do Songo ya Msumbiji kati ya Agosti 9 na 11 kabla ya kurejea nyumbani kwa mchezo wa marudiano kati ya Agosti 23 na 25.

Ikifanikiwa kuvuka raundi ya kwanza, Simba itakutana na mshindi kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi na ikifuzu mtihani huo pia itaingia tena hatua ya makundi.

Mabingwa hao wa Tanzania Bara walianza mechi zao za kujipima nguvu kwa kuifunga mabao 4-0 timu ya Chuo Kikuu cha Orbit Tvet, kabla ya kuwachapa wenyeji, Platinums Stars FC mabao 4-1 na ikatoka sare ya bao 1-1 na Township Rollers, mechi zote zikipigwa mjini Rusternburg.

Mchezo huo wa kesho utakuwa ni wanne wa kujipima nguvu kwa Simba katika kambi yake ya Afrika Kusini kujiandaa na msimu mpya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >